
NURU YA IMANI
FURAHA YA MOYO
Mkusanyaji na Mwandishi
TAHIR ALI MOH'D

YALIYOMO

UTANGULIZI.....4

UISLAMU, IMANI NA IHSAAN.....6

MAMBO YENYE KUTENGUA UISLAMU.....9

MAANA YA IMANI.....17

KUMUAMINI ALLAH.....20

DALILI ZA ALLAH KATIKA ULIMWENGU.....27

TAUHIDI.....35

KUAMINI MALAIKA.....41

KUAMINI VITABU.....47

KUIAMINI QUR'ANI.....47

KUAMINI MITUME….....53

MAISHA YA NABII MUHAMMAD.....56

KUAMINI SIKU YA MWISHO.....66

KUAMINI PEPO.....69

KUAMINI MOTO.....71

KUAMINI QADAR.....72

SIFA ZA WAUMINI.....73

NAFASI YA SWALA KATIKA UISLAMU.....75

MAMBO YA IMANI.....80
UTAMU WA IMANI.....86
FAIDA ZA IMANI.....91
HALI ZA MOYO WA MWANADAMU.....98
UDHAIFU WA IMANI.....101
ATHARI ZA MAASI.....106
MAASI YA MOYO.....108
MAASI YA ULIMI.....111
MADHAMBI MAKUBWA.....112
MADHAMBI MADOGO.....118
NJIA ZA KUYAFIKIA MAISHA MAZURI.....121
TOBA YA KWELI.....124
HAKI YA ALLAH.....127
HAKI ZA MTUME….....129
HAKI ZA MUISLAMU.....131
HAKI ZA WAZAZI.....133
HAKI ZA MKE NA MUME.....133
UJUMBE WA MWISHO.....138
DUA.....142
MAREJEO YA VITABU.....143

UTANGULIZI

Bismillaahi Rrahmaani Rrahiim

Kila sifa njema Anastahiki Allah ﷻ, Muumba, Mmiliki, Muendeshaji na Msimamiaji wa Ulimwengu wote. Rehma na Amani za Allah zimshukie Mtume wetu Muhammad ﷺ Aliyetumwa na Allah ili Awe rehma na mkombozi kwa viumbe vyote.

Allah ﷻ Amesema katika Qur'ani yake;

"Mwenye kufanya matendo mema akiwa mwanamme au mwanamke hali ya kuwa ni muumini [Mwenye Imani Sahihi], basi tutamfanya aishi maisha mazuri na kwa hakika tutawalipa huko Akhera malipo yao kwa uzuri zaidi ya yale mazuri waliokuwa wakiyafanya (duniani)"

Hakika **IMANI** ndiyo msingi wa maisha ya Muislamu. Imani humjenga Muislamu ndani na nje; humtia nuru moyoni, humwelekeza katika maamuzi, humfariji katika misukosuko na humuimarisha katika nyakati za neema na mitihani. Bila imani sahihi, ibada hukosa ladha, maisha hukosa mwelekeo na subira hupungua thamani.

Hakika **IMANI** ni pumzi ya roho na sauti ya matumaini katika moyo; inapokuwa imara, huzuni hulegea na hofu hupotea. Imani humfanya Muislamu atulie kwa kile anachomwamini Allah. Ni imani ndiyo inayobadilisha

machozi kuwa dua, maumivu kuwa daraja la ukaribu kwa Allah, na maisha ya kawaida kuwa ibada yenye maana.

Hakika **IMANI** ni nuru ya moyo na uhai wa roho; bila imani maisha huwa kivuli kisicho na mwelekeo. Imani humuinua Muislamu katika shida, humtuliza katika hofu, na humfanya aone rehma ya Allah hata akiwa katikati ya mitihani. Mwenye imani huishi kwa matumaini, hufa kwa utulivu, na hukutana na Mola wake akiwa na furaha ya kweli ya moyo uliosalimika.

Kitabu hiki kimeandaliwa ili kumkumbusha Muislamu nafasi ya imani katika safari yake ya duniani, na jinsi inavyokuwa ngao, dira na chemchem ya matumaini. Ni mwaliko wa kuirejesha imani katika moyo, kuikuza katika matendo na kuithibitisha katika kila hatua ya maisha, ili tupate radhi za Allah ﷻ duniani na akhera.

Tunamuomba Allah ﷻ akijaalie kitabu hiki kiwe miongoni mwa sababu za kuongeza na kulinda imani zetu, na kutuongoza kwenye njia iliyonyooka. Aamiin

TAHIR ALI MOH'D,

***binaly24434@gmail.com*,**

0773 274875 / 0716 673720

Digital Platform: Jiongezee Maarifa

16 Rajab,1447 B.H = 5 Jan 2026 B.I

BUBUBU, ZANZIBAR, TANZANIA

Bismillaahi Rrahmaani Rrahiim

UISLAMU, IMANI NA IHSAAN

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema “Hakika dini (ya haki) mbele ya Allah ni Uislamu” Qur’ani [3:19].

Allah ﷻ Amesema “Je wanataka (Mayahudi, Wakristo na Washirikina) dini nyengine isiyokuwa dini ya Allah (Subhanahu Wataala) nayo ni Uislamu hali ya kuwa wote walioko mbinguni na ardhini wamejisalimisha na kunyenyekea kwa Allah (Subhanahu Wataala) kwa hiari na kwa nguvu na kwake watarejeshwa Siku ya Kiyama (alipwe kila mtu alichofanya duniani)” Qur’ani [3:83].

Allah ﷻ Amesema “Na mwenye kutafuta (kufuata) dini (nyengine yoyote) isiyokuwa dini ya Uislamu, basi hiyo haitakubaliwa kwake, na yeye Akhera atakuwa ni miongoni mwa wenye kupata khasara (kwa kuzinyima nafsi zao mambo yenye kuzinufaisha)” Qur’ani [3:85].

Allah ﷻ Amesema “...Leo (Ijumaa, mwezi tisa, mfunguo tatu, mwaka wa kumi, baada ya Hijra) Nimekukamilishieni Dini yenu (Dini ya Uislamu, kwa kuuhakikishia ushindi na kuikamilisha sheria) na nimewatimizia neema zangu kwenu (kwa kuwatoa kwenye giza la ujinga na kuwapeleka kwenye

mwangaza wa imani) na nimewaridhia kwamba Uislamu ndio Dini, (basi shikamaneni nayo wala musiiache) ...” Qur’ani [5:3].

Nini Maana ya Dini?

Katika Uislamu, ***Dini*** *ni mfumo kamili wa maisha ya mwanadamu ambao msingi wake mkuu ni* ***kumuamini na kumuabudu Allah (Subhanahu Wataala) bila kumshirikisha na kitu chochote***. Wakati tunafahamu kuwa lengo kuu la kuumbwa Wanadamu na Majini ni kumuabudu Allah (Subhanahu Wataala),

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema:

“Sikuwaumba Majini na Watu isipokuwa waniabudu, Sihitaji kutoka kwao riziki (yoyote) wala sihitaji wanilishe, Hakika Allah (Subhanahu Wataala) ndiye Mwenye kuruzuku (viumbe vyote) Mwenye nguvu madhubuti” Qur’ani (51:56-58).

Kwa maana Allah (Subhanahu Wataala) Amemuumba mwanadamu na kumrahisishia kila anachohitaji katika maisha ili Amuabudu Yeye tu bila kumshirikisha na chochote. Muda wote na katika mambo yote mwanadamu akiwa katika utiifu na kunyenyekea kwa Allah (Subhanahu Wataala) ndio anakuwa yumo katika nidhamu na mfumo sahihi wa maisha anaoutaka na kuuridhia Allah (Subhanahu Wataala) na muda wote

atakaokataa kuwa mtiifu na kunyenyekea kwa Allah (Subhanahu Wataala) katika jambo lolote basi anakuwa anakwenda kinyume na nidhamu na mfumo sahihi wa maisha alioumbiwa na Mola wake.

Dini ya Uislamu Kwa Ujumla Imejengwa Juu Ya Nguzo au Mambo 12 Yaliyogawanywa katika Madaraja makuu matatu (3);1-UISLAMU (Nguzo 5), 2-IMANI (Nguzo 6) NA 3-IHSAAN (Nguzo 1):

Mambo hayo Ameyaeleza Mtume Swallallahu alaihi wasallam katika hadithi mashuhuri inayoitwa Hadithi ya Jibril ambapo Jibril Alimuuliza Mtume Swallallahu Alaihi Wasallam nini Uislamu? Nini Imani? Na nini Ihsaan? Mtume Swallallahu Alaihi Wasallam Akajibu kama itakavyofuata:

KWANZA-UISLAMU: Maana yake ni kujisalimisha (kunyenyekea) kwa Allah (Subhanahu Wataala) kwa kufuata kwa vitendo yale yote Aliyokuja nayo Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) kutoka kwa Allah (Subhanahu Wataala).

Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema katika Hadithi ya Jibril "Uislamu ni kushuhudia (kukiri kwa moyo na kutamka kwa ulimi) kwamba hakuna Mungu anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah (Subhanahu Wataala) na

kushuhudia kwamba Muhammad (Swallallahu Alaihi Wasallam) ni Mjumbe wa Allah (Subhanahu Wataala), Kusimamisha Swala tano (kwa kuchunga sharti na nguzo zake), Kutoa Zaka (kwa wanaostahiki), Kufunga (mwezi mtukufu wa Ramadhani) na Kuhiji katika Nyumba (Al-Kaaba) kwa mwenye uwezo (mara moja katika umri)" (Hadithi Sahihi).

MAMBO YENYE KUTENGUA UISLAMU

Wanachuoni Wamesema, Muislamu anatoka katika Uislamu kwa kufanya moja wapo ya mambo hatari yafuatayo:

[1]-Kumshirikisha Allah (Subhanahu Wataala) katika IBADA [Kuwaabudu viumbe badala ya Allah (Subhanahu Wataala) Anaestahiki kuabudiwa, kuombwa na kutegemewa na viumbe vyote].

[2]-Kuritadi (Kutoka kwa makusudi katika Uislamu) na kuchagua ima Uyahudi au Ukiristo au Umajusi au Umasonia n.k.

[3]-Kuamini kuwa sheria zisizokuwa za kiislamu (sheria za kitwaghuti) ni bora na zimekamilika zaidi kuliko sheria za Kiislamu [Sheria za Allah (Subhanahu Wataala)] zilizokuja katika Qur'ani Takatifu.

[4]-Kuamini kuwa mwenendo na muongozo usiokuwa wa Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) [mwenendo wa mayahudi, wakiristo, washirikina na wamasonia] ni bora na umekamilika zaidi kuliko mwenendo na muongozo sahihi wa Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam).

[5]-Kuchukia chochote katika mambo yote ya kheri Aliyokuja nayo Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) kutoka kwa Allah (Subhanahu Wataala).

[6]-Kumfanyia Istihizai (Inda) Allah (Subhanahu Wataala) au Dini yake [Uislamu] au Mtume wake [Muhammad (Swallallahu Alaihi Wasallam)] au Kitabu chake [Qur'ani Takatifu] na Mambo mengine matukufu ya Allah (Subhanahu Wataala).

[7]-Uchawi (na mambo yote ya uharibifu na ufisadi yanayoambatana na uchawi kama vile kuwatenganisha wanandoa na kuzigombanisha koo na familia).

[8]-Kuwasaidia makafiri na washirikina katika kuwapiga vita na kuwadhulumu Waislamu kwa namna yoyote.

[9]-Kutowakufurisha Makafiri yaani mtu kuamini kuwa hakuna ubaya kwa Makafiri kumpinga Allah Subhanahu Wataala na Mtume wake Swallallahu Alaihi Wasallam au kutia shaka juu ya ukafiri wao.

[10]-Kuudharau na kuupuuza Uislamu [kutojali na kutojishughulisha na chochote katika Uislamu si kujifundisha (mambo ya lazima), si kuufanyia kazi, si kuufundisha wala kuutetea na kuuhami mpaka inakuwa hakuna tofauti yoyote baina ya huyo anayejiita Muislamu na asiyekuwa Muislamu, wote sawa!]. Tunamuomba Allah (Subhanahu Wataala) Atukinge na mambo hayo, Aamiin.

PILI-IMANI: Maana yake ni ***Itikadi*** sahihi ya Moyoni na ***Matendo*** mema ya Viungo, inaongezeka (inathibiti) kwa kumtii Allah na inapungua (inadhoofika) kwa kumuasi Allah (Subhanahu Wataala).

Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema katika Hadithi ya Jibril "Imani ni kumuamini Allah (Subhanahu Wataala) [Kuamini kuwa Allah (Subhanahu Wataala) Yupo na ni Mmoja tu Ambae hana mshirika katika Uungu wake (Ibada/kuabudiwa), Vitendo vyake (Kuumba, kumiliki, kusimamia, kuruzuku, kuhuisha, kufisha, kufufua, kuhukumu n.k) na Majina na Sifa zake zote na hiyo ndio Tauhidi [Kumpwekesha Allah (Subhanahu Wataala) ambayo ndio Dini ya Mitume wote waliotangulia kabla ya Mtume wetu Muhammad Swallallahu Alaihi Wasallam],
Kuamini Malaika wake [Jibril, Mikael, Israfil,

Malaika wa mauti n.k], Kuamini Vitabu vyake [Taurati, Zaburi, Injili, Qur'an n.k], Kuamini Mitume yake [Nuh, Ibrahim, Musa, Isa, Muhammad n.k], Kuamini Siku ya Mwisho [Siku ya Kiyama na mambo yote yanayoambatana na siku hiyo nzito kuanzia mauti, neema na adhabu za kaburi, kufufuliwa, mezani, hesabu, uombezi, swirati, pepo, moto n.k] na Kuamini Qadar [Kheri na shari vyote vinatoka kwa Allah Subhanahu Wataala]" (Hadithi Sahihi).

Imani inakaa katika Moyo na inathibitishwa na Matendo Mema, kuongezeka kwa matendo mema ni dalili ya kuongezeka (kuthibiti) kwa imani na kupungua kwa matendo mema ni dalili ya kupungua (kudhoofika) kwa imani. Tunamuomba Allah (Subhanahu Wataala) Aithibitishe na Aipambe Imani katika nyoyo zetu, Aamiin.

Matendo Mema ya Imani yamegawika sehemu kuu tatu:
1-Matendo ya Moyoni kama vile kumkumbuka, kumtambua, kumuogopa, kumpenda, kumnyenyekea na kumtegemea Allah (Subhanahu Wataala) n.k.
2-Matendo ya Ulimi kama vile kutamka shahada mbili, kusoma Qur'ani, kumuomba na kumtaja Allah (Subhanahu Wataala), kuamrisha mema na kukataza maovu n.k.
3-Matendo ya Viungo vyengine kama vile

Kusimamisha Swala tano, Kutoa zaka, Kufunga, Kuhiji, Kulisha masikini, Kupigania dini ya Allah (Subhanahu Wataala) n.k.

Maasi yanayobatilisha Imani vile vile nayo yamegawika sehemu kuu tatu:

1-Maasi ya Moyo kama vile Shaka, Unafiki, Kibri, Husda, Kujiona, Kujionyesha, n.k.

2-Maasi ya Ulimi kama vile kusema uongo, kusengenya, kuamrisha uovu n.k.

3-Maasi ya Viungo vyengine kama vile kuua, kuzini, kuiba, kulewa n.k.

WANACHUONI WAMESEMA:

1-Nyumba ya Imani ni **MOYO** wa Muumini

2-Kichwa cha Imani ni **LAA ILAAHA ILLALLAH**

3-Roho ya Imani ni **TAUHIDI**

4-Kiini cha Imani ni **IKHLAS**

5-Mwili wa Imani ni **DHIKRI**

6-Moyo wa Imani ni **QUR'ANI**

7-Ubongo wa Imani ni **DUA**

8-Nuru ya Imani ni **SWALA**

9-Dalili ya Imani ni **SWADAKA**

10-Ngome ya Imani ni **SWAUMU**

11-Njia ya Imani ni **ELIMU**

12-Uhai wa Imani ni **SUBRA**

13-Matunda ya Imani ni **WEMA NA UCHAMUNGU**

HAYA ni sehemu muhimu katika sehemu za imani kwa kuwa inamzuia mja kufanya kila baya linalostahiki lawama. Haya haileti isipokuwa kheri tupu.

TAQWA (UCHAMUNGU) maana yake ni kutekeleza maamrisho yote Aliyoamrisha Allah na kuacha makatazo yote Aliyokataza Allah. Muislamu hawezi kuwa Mchamungu bila kuwa Muumini wa kweli.

Muislamu yeyote mwenye Imani ya kweli iliyotulia Moyoni kisha akawa Mchamungu Anakuwa ni Walii (Mpenzi) wa Allah Subhanahu Wataala.

Allah Subhanahu Wataala Amesema:

“Jueni (tambueni) kuwa hakika (Si vyenginevyo) mawalii (wapenzi) wa Allah ni wale ambao hawatokuwa na hofu wala hawatohuzunika. Wale wenye kumuamini Allah na wakawa Wachamungu” Qur’ani [10:62-63].

MATENDO YANAYO IMARISHA IMANI

1-Kuzingatia maana ya Majina na Sifa za Allah (Subhanahu Wataala),
2-Kuisoma Qur'ani kwa kuizingatia maana yake,
3-Kufanya wingi wa matendo ya Sunna baada ya Faradhi,
4-Kujishughulisha katika kutafuta elimu ya kumtambua Allah (Subhanahu Wataala),

5-Kumkumbuka na kumtaja Allah (Subhanahu Wataala) kwa wingi wakati wote,
6-Kusoma na kuzingatia Maneno na Maisha ya Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) na Watu wema waliotangulia pia kukaa katika vikao vya watu wema waliopo.

MAMBO YANAYO DHOOFISHA IMANI

1-Kuacha kumshukuru Allah (Subhanahu Wataala) juu ya neema ya Imani (Neema kubwa mno) kwa kupunguza matendo yanayozidisha Imani kama kusoma Qur'ani kwa kuizingatia maana yake, kumtaja sana Allah na mengineyo ambayo ndiyo yanayo imarisha na kuithibitisha Imani katika moyo. Imani ni rahisi sana kutoweka katika moyo iwapo Muislamu hatoichunga na kuithamini kwa kufanya juhudi ya kuiimarisha (kuizidisha) na kuilinda (kuihifadhi).
2-Kutoogopa kuondokewa na Imani kwa kutojiepusha na maasi ambayo ndiyo yanayoiondosha Imani katika moyo au kuifanya kuwa dhaifu mno kwa sababu Imani na maasi ni mambo ambayo hayawezi kabisa kukaa pamoja. Imani ikitawala katika moyo maasi yote yanaondoka na maasi yakitawala Imani inatoweka.
3-Dhulma yaani kuwadhulumu ndugu zako waislamu kwa namna yoyote kama kutowatimizia haki zao na kutosalimika na shari zako kwa kuvunja heshima zao na kumwaga damu zao.

TATU-IHSAAN: IHSAAN ndio daraja la juu la ukaribu baina ya mja na Mola wake. ***Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema katika Hadithi ya Jibril "IHSAAN ni Kumuabudu Allah (Subhanahu Wataala) kama kwamba unamuona [hapo utakuwa unamuabudu na kumnyenyekea Allah (Subhanahu Wataala) kwa kutarajia Rehema zake] na kama wewe humuoni basi Yeye Anakuona [na hapo utakuwa unamuabudu na kumnyenyekea Allah (Subhanahu Wataala) kwa kuogopa adhabu zake]".***

Ndugu/Dada yangu Muislamu, Allah Akurehemu Mambo hayo (Uislamu, Imani na Ihsaan) ni muhimu sana kwa Muislamu yeyote kuyafahamu angalau kwa ujumla kama yalivyoainishwa hapo kwa sababu *lisilopatikana lote huwa haliachwi lote*. Haina maana yoyote kwa mtu kujiita Muislamu halafu ikawa hajui chochote kuhusu Dini yake.

Katika mambo yote ya msingi anayotakiwa Muislamu kuyapa kipao mbele katika maisha yake, IMANI ndio jambo la mwanzo na muhimu zaidi na mambo yote yanatengenea kwa kutengenea Imani na yanaharibika kwa kuharibika au kudhoofika kwa Imani Sahihi. Tunamuomba Allah (Subhanahu Wataala) Aipambe Imani katika nyoyo zetu na Atuingize katika waja wake walioongoka Aamiin.

Bismillaahi Rrahmaani Rrahiim

MAANA YA IMANI

Imani ni nini? Imani ni ***Itikadi sahihi*** ya moyoni iliyothibitishwa na ***Matendo mema*** ya viungo, inaongezeka (inathibiti) kwa kumtii Allah (Subhanahu Wataala) na inapungua (inadhoofika) kwa kumuasi Allah (Subhanahu Wataala).

Kwa maana nyengine, Imani ni kuamini (kusadikisha) kwa moyo na kutenda kwa vitendo yale yote Aliyokuja nayo Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) kutoka kwa Allah (Subhanahu Wataala).

Kwa ufupi Imani ni Kumuamini Allah (Subhanahu Wataala) na kuamini mambo yote Aliyoamrisha Allah (Subhanahu Wataala) kuyaamini na kuyatenda.

Kama kweli Imani imethibiti katika moyo basi ni lazima athari yake itaonekana katika matendo mema. Kwa hivyo hakuna Imani bila matendo mema kama ambavyo hakuna matendo mema yenye ujira kwa Allah (Subhanahu Wataala) siku ya malipo bila Imani.

Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema “Imani ni Kumuamini Allah (Subhanahu Wataala) [Kuamini kuwa Allah (Subhanahu Wataala) yupo na ni mmoja tu ambae hana mshirika katika Uungu au ibada

(kuabudiwa), ufalme wake, vitendo vyake, majina yake, sifa zake na dhati yake na hiyo ndio Tauhidi (Dini ya Mitume wote waliotangulia)], Kuamini Malaika wake [Jibril, Mikael, Israfil, malaika wa mauti n.k], Kuamini Vitabu vyake [Taurati, Zaburi, Injili, Qur'an n.k], Kuamini Mitume yake [Nuh, Ibrahim, Musa, Isa, Muhammad (Swallallahu Alaihi Wasallam) n.k], Kuamini Siku ya mwisho [Siku ya Kiyama na mambo yote yanayoambatana na siku hiyo nzito kuanzia Mauti, neema na adhabu za kaburi, kufufuliwa, hesabu, Swirati, Pepo, Moto n.k] na Kuamini Qadar [Kheri, shari na vyote vinavyotokea vinatokea kwa mipango na makadirio maalum ya Allah (Subhanahu Wataala)].

Na kuhusiana na Uislamu, Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema “Uislamu ni kushuhudia [kukiri kwa moyo na kutamka kwa ulimi] kwamba hapana Mola anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah (Subhanahu Wataala) na kwamba Muhammad (Swallallahu Alaihi Wasallam) ni Mjumbe wa Allah (Subhanahu Wataala), kusimamisha Swala tano [kwa kuchunga sharti na nguzo zake], kutoa zaka [kwa wanaostahiki], kufunga [mwezi mtukufu wa Ramadhani] na Kuhiji katika Nyumba [Al-Kaaba] kwa mwenye uwezo [mara moja katika umri].

Ameitafsiri IMANI kwa Itikadi ya moyoni na UISLAMU kwa matendo ya wazi ya viungo.
Wanachuoni wengine wamesema “Imani ni nuru ya uongofu wa Allah (Subhanahu Wataala) Anayomtunukia mja wake kwa kuiingiza katika moyo wake ikamfanya amtambue, ampende, amuogope na amtegemee Mola wake. Kwa maana hii, Imani imegawika aina tatu: 1-Imani ya Malaika-Haizidi wala haipungui, wao daima hawamuasi Allah (Subhanahu Wataala) na wanafanya yote wanayoamrishwa bila kuchoka. 2-Imani ya Mitume-Inazidi tu haipungui kwa kuwa wao wanamtambua zaidi Allah (Subhanahu Wataala), Imani zao zinatofautiana kwa mujibu wa elimu na maarifa yao ya kumtambua Allah (Subhanahu Wataala).
3-Imani ya Waumini-Inaongezeka (inathibiti) kwa kumtii Allah (Subhanahu Wataala) na inapungua (inadhoofika) kwa kumuasi, Imani hii vile vile inatofautiana kwa mujibu wa namna mja anavyomtambua Allah (Subhanahu Wataala) na wenye Imani za juu zaidi baada ya Mitume wa Allah (Subhanahu Wataala) na wafuasi wao ni wanachuoni.
Allah (Subhanahu Wataala) Amesema: “...Hakika wanaomuogopa Allah (Subhanahu Wataala) [kwa kumtii na kujiepusha na kumuasi] katika waja wake ni Wanachuoni [wanaomtambua]...” Qur’ani [35:28].

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema katika Aya nyengine: "...Allah (Subhanahu Wataala) Anawainua daraja (vyeo) Waumini miongoni mwenu na Anawainua wale waliopewa Elimu daraja nyingi..." Qur'ani [58:11].

NGUZO ZA IMANI

Nguzo za Imani ni Sita, Allah (Subhanahu Wataala) Amezitaja kwa Kusema "…Lakini Wema uko kwa yule aliyemuamini Allah (Subhanahu Wataala) na (akaamini) Siku ya mwisho, na (akaamini) Malaika, (akaamini) Vitabu (vya Allah Subhanahu Wataala) na (akaamini) Mitume ya Allah (Subhanahu Wataala) …" Qur'ani [2:177]. Pia Qur'ani [2:285] na [4:136].

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema katika aya nyengine "Hakika kila kitu tumekiumba kwa Qadar (kwa mujibu wa elimu, matakwa na kile tulichokiandika katika Ubao Uliohifadhiwa)" Qur'ani [54:49].

Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema "Imani ni kumuamini Allah (Subhanahu Wataala), kuamini Malaika wake, kuamini Vitabu vyake, kuamini Mitume yake, kuamini Siku ya mwisho na kuamini Qadar, kheri na shari yake" [Hadithi Sahihi].

KUMUAMINI ALLAH

Hakika kumuamini Allah (Subhanahu Wataala) ndio nguzo kuu na muhimu zaidi katika nguzo za Imani na

maana ya kumuamini Allah (Subhanahu Wataala) ni kuamini kuwa Allah (Sunhanahu Wataala) Yupo na ni mmoja tu Ambae hana mshirika katika Uungu au kuabudiwa (Ibada), hana mshirika katika Vitendo vyake (Uumbaji, Uendeshaji, Usimamiaji na Ufalme wake) na hana mshirika katika dhati, majina na sifa zake zote. Kumuamini Allah (Subhanahu Wataala) ndio msingi mkuu wa dini na ibada zote kukubalika kwake zinategemea msingi huu mkubwa kwa maana ikitengenea (ikithibiti) imani, ibada zote zinatengenea kwa kuwa nyepesi na kukubalika mbele ya Allah (Subhanahu Wataala) na kuyafanya mahusiano ya mja na Mola wake kuwa mazuri na imani ikiharibika (ikidhoofika), ibada zinakuwa ngumu kutekelezeka na kukubalika mbele ya Allah (Subhanahu Wataala) na mahuhusiano yaliopo baina ya mja na Mola wake yanaharibika. Kumuamini Allah (Subhanahu Wataala) ndio Amali bora kuliko zote kama ilivyokuja katika hadithi sahihi. Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema baada kuulizwa Amali bora ni ipi ? “Kumuamini Allah (Subhanahu Wataala) na Mtume wake (Swallallahu Alaihi Wasallam)” [Sahihi].

Ili Muislamu kunufaika na imani [kumuamini Allah (Subhanahu Wataala)] juhudi (jitihada au bidii) za aina tatu zinahitajika muda wote katika maisha yake:

Juhudi ya kuitafuta (kuifikia) Imani : Hii ni juhudi ya kufanya mema kama vile kusimamisha swala tano khasa swala ya Alfajiri, kusoma Qur'ani kwa kuizingatia maana yake, kutoa kwa ajili ya Allah Subhanahu Wataala na matendo mengine ya kujieka karibu na Allah Subhanahu Wataala ya faradhi na sunna. Kila Muislamu Akihisi ugumu katika kuyaendea matendo mema basi hiyo ni ishara kuwa bado hajaifikia Imani inayotakiwa.

Juhudi ya kuihifadhi (kuilinda) Imani : Hii ni juhudi ya kujizuia na maasi yote makubwa na madogo ambayo yanaharibu mahusiano ya mja na Mola wake au yanamueka mbali mja na Mola wake.

Juhudi ya kuilingania Imani : Hii ni juhudi ya kuwausia na kuwahimiza ndugu zako waislamu mambo yote ya kheri yatakayo wafanya wawe karibu na Allah Subhanahu Wataala kwa njia yoyote.

Allah (Subhanahu Wataala) Amezieleza Juhudi hizo katika Sura fupi yenye maana kubwa sana ambayo ni Surat Al-Asr. Imaam Shafi Amesema kuhusiana na surah hii kuwa : Lau kama watu wataizingatia surah hii basi ingewatosha'' na kauli nyengine : ''Lau kama Qur'ani yote haikuteremshwa isipokuwa surah hii basi ingewatosha watu'' kutokana na ujumbe wake uliokusanya maagizo mazito ya Allah

Subhanahu Wataala yatakayomfanya Mwanadamu akasalimika na kuokoka na khasara ya kuangamia katika maisha yake ya duniani na maisha ya milele ya Akhera, Maisha yenye mwanzo lakini hayana mwisho.

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema katika Surat Al-Asr :

“Naapa kwa zama (wakati), Hakika mwanadamu (yeyote) yumo katika khasara (ya kuangamia), Isipokuwa (Hawamo katika khasara) wale walioamini (wenye imani ya kweli iliyotulia moyoni) na wakafanya matendo mema (kwa viungo vyao) na wakausiana kushikamana na haki (kheri zote) na wakausiana kushikamana na kusubiri (katika kutekeleza maarisho, kuacha makatazo, maradhi, misiba, mabalaa na maudhi ya watu)” [Qur’ani 103 :1-3]

Pia Allah Amesema katika Surat Al-Ankabuut :

“Na wale wanaojitahidi kwa ajili Yetu, kwa hakika tutawaongoza kwenye njia zetu. Na bila shaka Allah (Subhanahu Wataala) Yuko pamoja na wafanyao mema (kwa ajili Yake)” Qur’ani [29 :69].

Na kwa sababu Imani inaongezeka (inathibiti) kwa kumtii Allah (Subhanahu Wataala) na inapungua (inadhoofika) kwa kumuasi Allah (Subhanahu

Wataala), ni muhimu sana kuyatia akilini mambo yafuatayo ili kuthibitisha au kuhakiki imani zetu :

[1] Kuwa na yakini (uhakika) kuwa Muumbaji wa viumbe vyote ni Allah (Subhanahu Wataala) Pekee, kwa hivyo Arshi na ukubwa wake ni kitu mbele ya Allah (Subhanahu Wataala), mbingu saba na ukubwa wake ni vitu mbele ya Allah (Subhanahu Wataala), jua, dunia, mwezi, hewa, maji, bahari, milima, watu, majini, malaika, wanyama, samaki, ndege, wadudu na viumbe vyengine vyote ni vitu katika idadi ya vitu Alivyoumba Allah (Subhanahu Wataala). Kujua na kuyazingatia kwa kuyatia akilini mambo hayo yatatufanya tuufahamu utukufu, ukubwa, ufalme na nguvu za Allah (Subhanahu Wataala) hatimaye tutamuogopa kwa kutii amri zake na kujizuia na kumuasi.

[2] Kuwa na yakini (uhakika) kuwa Mmiliki, Muendeshaji na Msimamiji wa viumbe vyote ni Allah (Subhanahu Wataala). Kwa hivyo kila kitu kilichopo kikubwa sana au kidogo sana, kinachoonekana na kisichoonekana na vyenginevyo vyote havina uwezo wa kujiendesha wenyewe bali vinategemea muongozo na amri ya Allah (Subhanahu Wataala). Allah (Subhanahu Wataala) Ndiye Muendeshaji wa ulimwengu wote na Ndiye Mpangaji na Msimamiaji wa nidhamu za viumbe vyote. Ameumba macho na Ameyaumbia athari yake ya

kuona, Ameumba masikio na Ameyaumbia athari yake ya kusikia, Ameumba midomo na ndimi na Ameuumbia athari yake ya kuzungumza, Ameumba Jua na athari yake ya kuangaza, Ameumba moto na athari yake ya kuunguza, Ameumba mimea na athari yake ya kuzaa matunda na mengineyo. Allah (Subhanahu Wataala) ni Muweza wa kuondoa athari zote za viumbe vyake au kukifanya kiumbe chake kwenda kinyume na athari yake kama Alivyoufanya moto kuwa baridi na salama kwa Nabii Ibrahim (Alaihi Salaam) ilhali moto athari yake ni kuunguza !
Allah (Subhanahu Wataala) ni Mjuzi na muweza wa kila kitu.

DALILI ZA ALLAH KATIKA MWANADAMU

Dalili za kiakili zinazoonyesha kuwepo Allah (Subhanahu Wataala) ukitoa zile dalili za maandiko zilizokuja katika Qur’ani ni nyingi mno kwa sababu vitu vyote katika Ulimwengu unaoonekana vinashuhudia uwepo wa Allah (Subhanahu Wataala) akiwemo mwanadamu mwenyewe. Allah (Subhanahu Wataala) Amemuumba mwadamu katika umbile la kumtambua Muumba wake.

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema “Basi uelekeze [Ewe Mtume] uso wako katika Dini iliyosawasawa, ndio Umbile la Allah (Subhanahu Wataala)

Alilowaumbia watu (yaani Uislamu unawafikiana barabara na umbile la Mwanadamu). Hakuna mabadiliko katika maumbile ya viumbe vya Allah (Subhanahu Wataala). Hiyo ndio Dini iliyonyooka, lakini watu wengi hawajui" Qur'ani [30:30].

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema "Je wanataka (Mayahudi, Wakristo na Washirikina) dini nyengine isiyokuwa dini ya Allah (Subhanahu Wataala) nayo ni Uislamu hali ya kuwa wote walioko mbinguni na ardhini wamejisalimisha na kunyenyekea kwa Allah (Subhanahuu Wataala) kwa hiari na kwa nguvu na Kwake watarejeshwa Siku ya Kiyama (alipwe kila mmoja alichofanya duniani)" Qur'ani [3:83].

Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema "Kila anayezaliwa anazaliwa katika umbile la (kumtambua) Allah (Subhanahu Wataala), wazazi wake ndio humfanya ima awe Myahudi [katika wafuasi wa Nabii Musa (Alaihi Salaam) waliokwenda kinyume na mafunzo yaliyomo katika Taurati iliyoteremshwa kwa Mtume wao] au Mnaswara [katika wafuasi wa Nabii Isa (Alaihi Salaam) waliokwenda kinyume na mafunzo yaliyomo katika Injili iliyoteremshwa kwa Mtume wao] au Mmajusi [katika wafuasi wanaoabudu moto, jua, mawe, miti na kadhalika] kama anavyozaliwa mnyama huzaliwa mnyama kamili aliyekamilika Jee munahisi

kuna kasoro yoyote (kwa huyo mnyama aliyezaliwa)?” [Hadithi Sahihi].

DALILI ZA ALLAH KATIKA ULIMWENGU

Namna Allah (Subhanahu Wataala) Alivyouumba na kuupamba Ulimwengu, Mtu yeyote mwenye akili na macho anafahamu kuwa yupo Muumba, Mfalme, Mmiliki, Muendeshaji na Msimimiaji. Ulimwengu wote huu unaojulikana (Observable Universe) na vitu vyote vilivyomo ndani yake katika vitu vilivyo karibu na mwanadamu katika sayari ya dunia kama vile wanyama, mimea, milima, bahari na vile vilivyo mbali na mwanadamu kama vile mwezi, sayari, jua, nyota n.k vyote hivyo vina Muumba Aliyeviumba, Mmiliki Anayevimiliki, Msimamiaji Anayevisimamia na Muendeshaji Anayeviendesha kwa utaratibu maalum, na ni jambo lisilowezekana na kuingia akilini kuwa ulimwengu wote huu na msongamano wa vitu vyake vingi namna hiyo viwe havina muumbaji, mmiliki, muendeshaji na msimamiaji, ikiwa meli tu yenye mizigo haiwezi kusimama wenyewe bandarini na kushusha au kupakia wenyewe mizigo bali inahitaji wasimamiaji kadhaa waliobobea na wazoefu ili kushusha au kupakia salama mizigo yote bila kutokea khitilafu yoyote, Jee huu ulimwengu wote na vyote

vilivyomo utawezaje kujiendesha wenyewe bila Msimamiaji mwenye nguvu na uwezo mkubwa wa kukipa kila kitu katika mabilioni ya vitu mahitaji yake ili kiende sawa kwa mpango bila maharibiko yoyote. Nidhamu ya ulimwengu ambao ni mkubwa mno kwa wanadamu, inahitaji usimamizi mkubwa zaidi kuliko meli ya mizigo! Hebu angalia sayari ya dunia pekee iliyojaa viumbe baharini na nchi kavu kama vile wanadamu, wanyama, ndege, wadudu, samaki, mimea n.k. kila kiumbe kina mahitaji yake maalum ambapo bila usimamizi madhubuti wa Yule Aliyeviumba na kuvipa mahitaji yake, kungetokea maharibiko na khitilafu nyingi.

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema “Ametakasika (Mola) Ambae Ameumba mbea (namna) mbili (kiume na kike) katika vitu vyote, katika vile ivioteshavyo ardhi (katika mimea), na katika nafsi zao (wanadamu), na katika vile wasivyovijua. Na usiku ni alama kwao (ya kuonyesha uwezo, utukufu na neema za Mola wao), tunauvua humo mchana, mara wanakuwa gizani. Na Jua (pia ni alama kwao), linakwenda (linazunguka) mpaka kituoni pake. Hayo ni makadirio (mipango) ya [Allah (Subhanahu Wataala)] Mwenye nguvu (uwezo wa kila kitu) na Mjuzi (wa vitu vyote). Na Mwezi (kadhalika ni alama kwao), Tumeupimia vituo, mpaka unakuwa (mwembamba) kama chaparare la mtende kukuu

(lililonywea). Haliwi jua kuufikia mwezi wala usiku kuupita mchana (ukaja kwa ghafla kabla ya wakati wake), na vyote (dunia, mwezi na jua) vinaogelea katika njia (orbits) zao (bila kuingiliana)" Qur'ani [36:36-40].

UCHAMBUZI:

🪐 ***ULIMWENGU***: Ulimwengu unajumuisha vitu vyote Alivyoumba Allah (Subhanahu Wataala) vile vinavyoonekana na visivyoonekana, vikubwa na vidogo, vilivyo mbali na vilivyo karibu vyote vinahesabika kuwa ni sehemu ya ulimwengu yaani kwa ufupi ni kila kitu kilichopo ukimtoa Allah (Subhanahu Wataala). Huu unaitwa Ulimwengu Wote (Entire Universe) ambao hakuna mwanadamu yeyote anayeweza kuujua ukubwa wake isipokuwa Yule Aliyeuumba pekee ambae ni Allah (Subhanahu Wataala) na ule ulimwengu ambao mwanadamu mpaka sasa ameweza kuupima na kuujua ukubwa wake kwa kutumia darubini na vipima anga, unaitwa Ulimwengu Unaoonekana/Unaojulikana (Observable Universe) ambao ni sehemu ndogo mno ya Ulimwengu Wote.

Kwa hivyo sayari yetu ya dunia (Earth) ni sehemu ndogo mno ya mfumo wote wa Jua (Solar System), Mfumo wa Jua nao ni sehemu ndogo mno ya mkusanyo wote wa kundi la nyota la Milky Way Galaxy. Milky

Way Galaxy nayo ni sehemu ndogo mno ya Ulimwengu unaoonekana (Observable Universe). Ulimwengu unaoonekana/unaojulikana nao ni sehemu ndogo mno ya Ulimwengu Wote (Entire Universe) na Muumba, Mmiliki, Muendeshaji na Msimamiaji wa huu Ulimwengu Wote ni Allah (Subhanahu Wataala).

Katika vitu Alivyoumba Allah (Subhanahu Wataala), Ameumba mbea au aina mbili katika vitu vyote: Hii ina maana kuwa vitu vyote vinavyoonekana katika Wanadamu, wanyama, mimea, matunda na vitu vyengine vingi ambavyo wanadamu kwa sasa hawavijui vimeumbwa mbea (namna) mbili kama Alivyosema Allah (Subhanahu Wataala) katika aya nyengine kuwa “Na katika kila kitu tumeumba mbea (aina) mbili ili mupate kukumbuka (Uwezo na Utukufu wa Mola wenu)” Qur’ani [51:49].

🌍 ***USIKU NA MCHANA***: Ni katika dalili kubwa za kuwepo Allah (Subhanahu Wataala). Usiku na mchana unafanyika kwa amri ya Allah (Subhanahu Wataala) pale sayari ya dunia inapojizungusha wenyewe wakati inalizunguka jua, upande wa dunia unaolielekea jua unakuwa mchana na upande mwengine wa dunia ambao haupati mwangaza wa jua unakuwa usiku, usiku unaingia taratibu kama unavyoingia mchana katika

maeneo tofauti katika mgongo wa ardhi kwa sababu ya umbile la mviringo la sayari ya dunia.

🌍 ***DUNIA (EARTH)***: Ni moja katika ***Sayari (Planets)*** zinazounda ***mfumo wa Jua (Solar System)*** yenye upana wa takriban kilomita 13,000 au meli 8,000.
Dunia ndio sayari pekee katika mfumo wa jua inayoishi viumbe hai kwa kuwepo mahitaji muhimu ya uhai kama vile hewa safi, maji na mimea. Dunia inachukua mwaka mzima (siku 365 na robo) kukamilisha mzunguko wake kulizunguka jua kwa kasi ya kilomita 108,000 kwa saa, sawa na meli 70,000 kwa saa na inachukua masaa 24 kukamilisha kujizungusha wenyewe. Wakati Mwezi unaizunguka dunia, dunia pamoja na Sayari nyengine katika mfumo wa jua inalizunguka jua, jua nalo pamoja na mabilioni ya nyota nyengine huzunguka kuizunguka sehemu ya kati ya mkusanyo mkubwa wa nyota unaoitwa “Milky Way” na inakadiriwa kuwa Jua huchukua miaka milioni 230 kukamilisha mzunguko wake kwa kasi ya meli 150 kwa sekunde. Dunia vile vile Allah Subhanahu Wataala Ameiekea matabaka ya hewa yanayoikinga na miale hatari ya jua pamoja na vipande vinavyokuja kwa kasi kutoka angani na kila tabaka lina kazi yake maalum kwa ajili ya kuifanya dunia iwe sehemu nzuri na salama ya kuishi viumbe.
Mpaka sasa hakuna sehemu nyengine yoyote popote katika Ulimwengu inayojulikana kuwepo viumbe hai

sio katika miezi na sayari za mfumo wa jua au sayari zilizopo nje ya mfumo wa jua (Exoplanets).

☽ ***MWEZI (MOON)***: Gimba lililo karibu zaidi na sayari ya dunia katika anga, upana wake ni kilomita 3,500 au meli 2,170, umbali unaoitenganisha dunia na mwezi ni meli 238,855 au kilomita 384,400. Kwa mujibu wa tafiti za wanasayansi na mafunzo ya Qur'ani, ni kuwa Mwezi haotoi mwangaza wake mwenyewe bali unaakisi (reflect) mwangaza wa jua (Tazama Qur'ani Sura ya71 Aya ya 16). Mwezi unaizunguka dunia na unachukua wastani wa siku 29 kukamilisha mzunguko wake. Wakati mwezi unaizunguka dunia, dunia nayo hujizungusha wakati inalizunguka jua hali ambayo husababisha muonekano wa mwezi kwa wakaazi wa duniani kubadilika kwa mujibu wa sehemu utakapokuwa. Mwezi hauonekani kabisa iwapo sehemu ya mwezi inayoangaziwa na jua haionekani kabisa na huu kwa kitaalamu unaitwa "new moon" na unaonekana wote iwapo sehemu ya mwezi inayoangaziwa na jua inaonekana yote na huu unajulikana kama "full moon" na baadhi tu ya sehemu ya mwezi inaonekana iwapo mwangaza wa jua unaangazia baadhi tu ya sehemu ya mwezi. Muonekano huu wa maumbile tofauti ya mwezi kutoka duniani katika Qur'ani umeashiriwa kwa neno la kiarabu "Manaazilal Qamar-Vituo vya Mwezi" na muonekano

huu huu unajulikana kama “Moon Phases’’ Awamu za Mwezi ambapo unabadilika na kuwa tofauti katika kila siku katika wastani wa siku 28 za mwezi mzima.

☀***JUA (SUN)***: Ni moja katika mabilioni ya ***Nyota (Stars)*** katika anga lenye upana wa kilomita 1,400,000 au meli 865,000 (zaidi ya dunia milioni moja zinaingia ndani yake), nalo kama nyota nyengine lina mwangaza na mwendo wake wenyewe, nalo linatembea kwa kasi ya kilomita 220 kwa sekunde. Jua ni tofauti na nyota nyengine katika anga kwa sababu lipo karibu zaidi na dunia, umbali unaolitenganisha jua na dunia ni takriban meli 93,000,000 au kilomita150,000,000, ukubwa na umbali huu ni mkubwa mno kwa mwanadamu lakini ni mdogo mno ukilinganisha na ukubwa na umbali unaolitenganisha jua na nyota nyengine katika anga ambapo umbali wa masafa makubwa kama hayo hupimwa kwa kutumia kasi ya mwangaza (meli 186,000 kwa sekunde moja), kwa kasi hii mwangaza unaweza kuizunguka dunia yote mara saba ndani ya sekunde moja tu!, kwa mwaka mzima mwangaza husafiri umbali wa takriban meli 6,000,000,000,000.
Umbali unaolitenganisha Jua na Nyota iliyo karibu zaidi inayoitwa Proxima Centauri ni miaka minne ya mwangaza yaani mwangaza wa jua unaochukua dakika nane tu kutufikia utachukua zaidi ya miaka minne kuifikia Proxima Centauri. Jua na sayari zake zote

ikiwemo dunia na mwezi wake vinaelea katika anga kwa mwendo maalum, mvutano maalum na kuelekea njia maalum. Na inajulikana kuwa jua na mkusanyo wake pamoja na mabilioni ya nyota zilizo karibu yake zipo katika mkusanyo mkubwa wa nyota uliotanda katika anga unaoitwa “The Milky Way” nao ni mmoja katika mabilioni ya mikusanyo au makundi ya nyota (Galaxies) yaliyopo katika anga na ule ulio karibu zaidi na mkusanyo wetu unaitwa “Andromeda” ambapo imekadiriwa kuwa mwangaza huchukua zaidi ya miaka milioni mbili na nusu kutoka katika mkusanyo wetu kuufikia, na imebainika kuwa sehemu zote za hiyo Milky Way Galaxy zinaizunguka sehemu ya kati yake kwa kasi ya kunasibiana na kinyume cha umbali wake kutoka hapo kati. Ukijumuisha idadi ya nyota zote zilizomo katika mikusanyo yote hiyo unapata idadi kubwa ya nyota kuliko chembe/changarawe/punje zote za mchanga uliopo duniani! Najua hutoamini kwanza lakini huo ndio ukweli ulivyo. Hebu angalia wingi huo wa nyota zilizopo katika anga kisha angalia ukubwa wa kila nyota halafu angalia masafa yaliyopo baina ya nyota moja na nyengine utaona namna gani ulimwengu huu ulivyokuwa mkubwa.

Ametakasika na Ametukuka Allah (Subhanahu Wataala) Mbora, Mfalme na Bwana wa waumbaji, wamiliki, waendeshaji na wasimamiaji wa mambo.

TAUHIDI

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema “Kwa jina la Allah (Subhanahu Wataala), Mwingi wa rehema (Rehema zilizokienea kila kitu katika ulimwengu) Mwenye kurehemu (kuwarehemu waja wake wema waliomuamini), Sifa na Shukrani zote njema Anastahiki Allah (Subhanahu Wataala) Mola [Muumba, Mmiliki, Muendeshaji na Msimamiaji) wa viumbe vyote kama vile watu, majini, malaika, wanyama, wadudu, ndege, samaki, mimea, bahari, milima, ardhi, mwezi, sayari, nyota na vyote vilivyopo ukimtoa Muumba Ambaye ni Allah (Subhanahu Wataala) pekee], Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu, Mfame na Mwenye kuimiliki Siku ya Malipo (Siku ya Kiyama), Wewe tu ndiye tunayekuabudu (kwa kuwa hakuna anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Wewe tu) na Wewe tu ndiye tunayekuomba msaada (katika mambo yetu yote ya duniani na akhera), Tuongoze katika njia iliyonyooka (Uislamu), Njia ya wale Uliowaneemesha (katika Mitume na Watu wema), Sio njia ya wale walioghadhibikiwa (kwa kuijua haki na kuikataa ambao ni Mayahudi na wanaowafuata) wala wale waliopotea (Wakiristo na wanaowafuata katika upotofu)” Qur’ani [1:1-7]. Hiyo ni Surat Al-Faatiha, Sura ya ufunguzi (utangulizi) katika Qurani tukufu. Pia

inaitwa Sura ya Swala, Mama wa Qur'ani na Aya Saba zenye kusomwa sana kwa kurudiwa kila mara.

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema "Sema, Ewe Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam); Yeye Allah (Subhanahu Wataala) ni Mmoja (katika kustahiki kuabudiwa, uumbaji, uendeshaji, usimamiaji na utakatifu wa majina na sifa zake hana mshirika katika hayo), Allah (Subhanahu Wataala) pekee ndiye Anayekusudiwa na waja kwa kukidhi haja na matakwa yao, Hakuzaa (Hana mwana wala mke) wala Hakuzaliwa (Hana mzazi), wala hakuna yeyote katika viumbe vyake vyote Alivyoviumba aliyefanana na Yeye (katika uungu wake, vitendo vyake, ufalme wake, majina na sifa zake)" Qur'ani [112:1-4].

Hiyo ni Surat Al-Ikhlas ambayo kwa jina jengine inaitwa Surat At-Tauheed yaani sura yenye maudhui ya kumpwekesha Allah (Subhanahu Wataala) katika Uungu wake (Ibada), Vitendo (Uwezo wake), Majina na Sifa zake zote bila kumshirikisha au kumfananisha na kiumbe chochote katika viumbe vyake.

AINA ZA TAUHIDI

Tauhidi maana yake ni kumpwekesha Allah (Subhanahu Wataala) katika Uungu wake (Ibada), Matendo yake na Majina na Sifa zake zote. Tauhidi

ndio Mila au Njia au Dini ya Mitume wote waliotangulia kabla ya Mtume wetu Muhammad Swallallahu Alaihi Wasallam.

Wanachuoni kwa kutumia mwangaza wa Qurani na Hadithi Sahihi za Mtume Swallahu Alaihi Wasallam Wameigawa Tauhidi katika aina kuu tatu;

TAUHID AR-RUBUUBIYYAH

Ni kumpwekesha Allah (Subhanahu Wataala) katika Vitendo vyake kwa kuamini kuwa hakuna mwenye kuumba, kumiliki, kusimamia, kuruzuku, kuhuisha, kufisha, kuhukumu, kukadiria na kadhalika isipokuwa Allah (Subhanahu Wataala) pekee na kinyume chake ni kumshirikisha Allah (Subhanahu Wataala) kwa kuamini kuwa wapo wengine wenye uwezo kama wa Allah (Subhanahu Wataala) wa kuumba, kuruzuku, kuhuisha, kufisha na kadhalika.

Aina hii ya Tauhidi wanaiamini Makafiri wengi na Washirikina ukiwatoa baadhi tu waliodai kuwa wao ni Waungu kama Firauni na Namrud ambao wao walitangaza wazi kuwa hakuna mungu yeyote isipokuwa wao.

Lakini hata hao washirikina wanaoamini kuwa Yupo Allah (Subhanahu Wataala) na Ndiye Aliyeumba kila kitu haliwafanyi hilo waingie katika Uislamu kwa kuwa

wanamshirikisha Allah (Subhanahu Wataala) katika Ibada [Wanawaabudu wengine badala ya Allah (Subhanahu Wataala) Anayestahiki kuabudiwa pekee].

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema “Sema Ewe Mtume kuwaambia makafiri; Ni Nani anayekuruzukuni kutoka mbinguni (kwa kuleta mvua) na katika ardhi (kwa kuotesha mimea)? Na nani anayemiliki masikio (yenu) na macho (yenu)? Na nani anayemtoa mzima katika mfu na akamtoa mfu katika mzima? Na nani anayetengeneza na kusimamia mambo yote?” Watasema; “Ni Allah” Basi sema “Je! Hamuogopi? (kwa kuwaabudu wengine wasiostahiki na kumuacha Yeye Anaestahiki Kuabudiwa?)” Qur’ani [10:31].

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema “Sema Ewe Mtume kuwaambia makafiri; Ni Nani Mmiliki wa ardhi (dunia) na vyote vilivyomo ndani yake ikiwa nyinyi munajua? Watasema “Ni Allah” Sema Je hilo haliwafanyi mukumbuke kuwa Yeye Allah ni Muweza wa kila kitu? Sema tena kuwaambia; Ni Nani Mola (Muumba, Mmiliki, Muendeshaji na Msimamiaji) wa mbingu saba na Mola wa Arshi iliyo kubwa? Watasema “Ni Allah” Sema Je hilo haliwafanyi muogope Adhabu ya Allah? Sema tena kuwaambia; Ni Nani Ambae Mikononi mwake kuna hazina za kila kitu na Yeye ni mwenye kulinda (kuhami) na hakilindwi chochote juu

yake, ikiwa mnajua? Watasema “Ni Allah” Sema kwa nini munadanganywa mukaacha kumuamini na kumtii Allah? Qur’ani [23:84-89].

Kwa hivyo sio kila anaekiri na kuamini uwepo wa Allah (Subhanahu Wataala) ni Muislamu, Wengi wa watu hawapingi uwepo wa Allah (Subhanahu Wataala) bali wanamshirikisha Allah katika Ibada yaani kwa kuwaabudu wengineo Asiyekuwa Yeye.

TAUHID AL-ULUUHIYYAH

Kumpwekesha Allah (Subhanahu Wataala) katika Ibada kwa kuamini kuwa hakuna anayestahiki kuabudiwa kwa haki katika aina zote za ibada isipokuwa Allah (Subhanahu Wataala) Pekee na kinyume chake ni kumshirikisha Allah (Subhanahuu Wataala) kwa kuamini kuwa wapo wengine wanaostahiki kuabudiwa kama vile kuabudu masanamu, jua, moto, mawe, kuwaomba maiti, masharifu na mengineyo ambayo hayastahiki kuabudiwa. Aina hii ya Tauhidi ndiyo wanayoipinga washirikina wote wa zama zote.

Allah (Subhanahuu Wataala) Amesema kuhusiana na aina hii ya Tauhid “Allah Hapana Mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye tu Aliye hai na Msimamizi wa mambo yote” Qur’ani [2:255].

“Na Mola wenu (Anayestahiki kuabudiwa kwa haki) ni Mola Mmoja tu, hapana Mola mwengine yeyote isipokuwa Yeye tu Mwingi wa rehema na mwenye kurehemu” Qur’ani [2:163].

“Hakika Mimi ndiye Allah (Subhanahu Wataala). Hapana Mola mwengine yeyote anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mimi tu, Basi niabudu Mimi na Usimamishe Swala kwa kunikumbuka Mimi” Qur’ani [20:14].

TAUHID AL-ASMAAU WASSWIFAAT

Kumpwekesha Allah (Subhanahu Wataala) katika majina na sifa zake zilizokuja katika Qur’ani na Hadithi sahihi bila kumfananisha au kumlinganisha na kiumbe chochote na kinyume chake ni kumshirikisha Allah (Subhanahu Wataala) kwa kufananisha sifa au jina lake na kiumbe chengine, kama kumpa kiumbe sifa ya elimu ya ghaibu (mambo yaliyofichikana) ambayo hakuna anaeyajua isipokuwa Allah (Subhanahu Wataala).

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema kuhusiana na aina hii ya Tauhid “Sema: Mwombeni Allah (Subhanahu Wataala) kwa jina la Allah (Muabudiwa wa Haki) au Mwombeni kwa jina la Rahmaan (Mwingi wa Rehema) au kwa jina lolote mtakalomwita, kwani Yeye anayo majina mazuri….” Qur’ani [17:110].

“Yeye ndiye Allah (Muabudiwa wa haki) Ambae hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Yeye tu, Al-Malik (Mfalme wa kweli), Al-Qudduus (Mtakatifu wa kweli), As-Salaam (Mwenye Amani), Al-Muumin (Mtoaji Amani kwa Waumini), Al-Muhaimin (Mwenye kuyaendesha Mwenyewe mambo Yake), Al-Aziiz (Mwenye Nguvu), Al-Jabbaar (Mwenye kufanya Analotaka), Al-Mutakabbir (Mkubwa Asiyeshindwa). Ametakasika Allah (Subhanahu Wataala) na hayo wanayomshirikisha nayo” Qur’ani [59:22-23].

KUAMINI MALAIKA

Kuamini Malaika ni kuamini kuwa Malaika ni viumbe katika viumbe wa Allah (Subhanahu Wataala) walioumbwa kwa nuru na kupewa nguvu na uwezo mkubwa wa kujigeuza katika maubile mazuri. Allah (Subhanahu Wataala) Amewapa uwezo mkubwa wa kusafiri kwa haraka na hakuna anayejua wingi wao isipokuwa Yeye. Allah (Subhanahu Wataala) Amewaumba kwa lengo la kumtumikia, kumuabudu na kusimamia mambo yake, hivyo hawana sifa za wanadamu na majini kama vile kula, kunywa, kuzaa, si wanaume si wanawake, makaazi yao ni mbinguni na hawamuasi Allah (Subhanahu Wataala) na wanafanya yote wanayoamrishwa bila kuchoka.

Malaika ni majeshi katika majeshi ya Allah (Subhanahu Wataala). Allah (Subhanahu Wataala) Amewapa majukumu na vyeo tofauti kulingana na uwezo wao pia Akawapa uwezo wa kuyatekeleza majukumu yao kwa ukamilifu bila kuchoka.

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema “Sifa njema zote ni zake Allah (Subhanahu Wataala) Muumba na muanzilishi wa mbingu na ardhi, Mwenye kuwafanya Malaika kuwa Wajumbe (kwa Mitume yake) Wenye mbawa mbili mbili, tatu tatu na nne nne [za kurukia ili kutekeleza walichoamrishwa na Allah (Subhanahu Wataala)]. Katika uumbaji wake Anaongeza Anachotaka. Hakika Allah (Subhanahu Wataala) ni muweza wa kila kitu. Qurani [35:1].

KAZI ZA MALAIKA

Baadhi ya Malaika na kazi zao waliotajwa katika Qur’ani Tukufu na Hadithi Sahihi ni hawa:

JIBRIL; Malaika mwenye kazi ya kuteremsha Wahyi (ujumbe) kutoka kwa Allah (Subhanahu Wataala) kwenda kwa Mitume yake. Allah (Subhanahu Wataala) Amesema “Ameshuka nayo (Qur’ani) Mhuisha sheria muaminifu (Jibril). Akakusomea mpaka ukaikusanya moyoni mwako ili upate kuwa mmoja wa waonyaji.

Ameshuka nayo kwa lugha ya kiarabu yenye maana iliyo wazi” Qur’ani [26:193-195].

MIKAIL; Malaika mwenye kazi ya kuteremsha mvua na kuotesha mimea katika ardhi.

ISRAFIL; Malaika mwenye kazi ya kupuliza Baragumu la kufisha na kufufua viumbe.

MALAIKA WA MAUTI; Malaika mwenye kazi ya kutoa roho za waja wakati wa mauti. Idara yake ina Malaika wa aina mbili, Malaika wanaotoa roho za Waja wema kwa upole na Malaika wanaotoa roho za Waja waovu kwa ukali na kishindo. Allah (Subhanahu Wataala) Amesema “Sema Ewe Mtume kuwaambia Makafiri na Washirikina; Atakaewafisha nyinyi ni Malaika wa kifo aliyewakilishwa kwenu (Atakayezichukua roho zenu utakapokwisha muda wenu wa kuishi) kisha mtarudishwa kwa Mola wenu (Akulipeni matendo yenu). Qur’ani [32:11].

MAALIK; Malaika mwenye kuusimamia Moto pamoja na Wasaidizi wake. Allah (Subhanahu Wataala) Amesema “Na Wataita Makafiri baada Allah (Subhanahu Wataala) Kuwatia kwenye moto wa jahannam; Ewe Maalik! Basi na Atufishe Mola wako, tupate kupumzika na haya tuliyonayo katika adhabu, Hapo Maalik Atawajibu; Hakika nyinyi ni wenye kukaa

(milele) motoni (hamna kutoka wala kukimbia)” Qur’ani [43:77].

Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema “Nimewaona usiku (wa Isra) watu wawili wamenijia wakasema; Yule Anayeukoleza moto ni Maalik (Msimamizi wa moto), na Mimi ni Jibril na huyu ni Mikail” [Hadithi Sahihi].

Malaika Mwenye kuisimamia Pepo pamoja nawasaidizi wake. Allah (Subhanahu Wataala) Amesema “Na wataongozwa wale waliomcha Mola wao (kwa kufuata maamrisho na kuacha makatazo) kuelekea Peponi, makundi kwa makundi. Na watakapoifikia na kufunguliwa milango yake (wataombwa waingie) na Malaika waliowakilishwa kuisimamia watawaambia; Amani iwe juu yenu! Hali zenu ni nzuri, Basi ingieni mukae milele” Qur’ani [39:73].

Malaika Mwenye kazi ya kumsimamia mtoto katika tumbo la mama baada kutimia miezi minne kwa kuandika riziki yake, ajali yake, vitendo vyake na kwamba atakuwa mwema au muovu.

Malaika Wenye kazi ya kuandika na kuhifadhi matendo ya Waja. Malaika wa kuliani anaandika mema na Yule wa kushoto anaandika maovu.

MUNKAR NA NAKIR; Malaika Wenye kazi ya kumuuliza maswali Mja mara anapoingizwa kaburini. Maswali anayoulizwa mja anapoingizwa kaburini ni Nani Mola wako? Ipi Dini yako? na Nani Mtume wako? Mja akiwa ni Muumini ataweza kuyajibu maswali hayo na atasalimika na adhabu, ama akiwa kafiri au mnafiki atashindwa na ataadhibiwa.

Malaika Wenye kuibeba Arshi ya Allah. Allah (Subhanahu Wataala) Amesema "…Na Wataibeba Arshi ya Mola Wako juu yao Siku ya Kiyama Malaika nane (miongoni mwa Malaika wakubwa)" Qur'ani [69:17].

Malaika wa majabali, hawa ni wale waliokuja kutaka kumsaidia Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) kuwaangamiza watu wa Twaif baada kumtukana na kumpiga mawe, Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallah) Akasema "Bali natarajia kuwa Allah (Subhanahu Wataala) Atatoa katika kizazi cha watu hawa wale watakaomuabudu Allah (Subhanahu Wataala) bila kumshirikisha na chochote" [Hadithi Sahihi].

Malaika Wenye kuizuru Baitul Maamuur; Nyumba ya Allah (Subhanahu Wataala) iliyopo mbingu ya saba kwa usawa wa Al-Kaaba inayotembelewa na Malaika wakati wote. Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema "Kisha ikainuliwa kwa ajili yangu Baitul

Maamuur, nikasema; Ewe Jibril! Hii ni Nini? Akasema; Hii ni Baitul Maamuur kila siku wanaingia ndani yake Malaika Sabiini Elfu, Wanapotoka hawarejei tena wale walioingia (bali huingia wengine)" [Hadithi Sahihi]. Wanachuoni wengine wanasema Baitul Maamuur ni Al-Kaaba iliyopo Makka ila kauli ya mwanzo ndio yenye nguvu zaidi na iliyothibitishwa kwa Hadithi Sahihi.

Katika kuamini Malaika Muumini hufahamu mambo yafuatayo:

Nguvu, Uwezo na Ukubwa wa Allah (Subhanahu Wataala) kwa sababu nguvu, uwezo na ukubwa wa kiumbe unafahamisha nguvu, uwezo, ukubwa na ufalme wa Muumba Ambae ni Allah (Subhanahu Wataala) ikiwa Malaika ambao ni viumbe katika viumbe wa Allah (Subhanahu Wataala) wana uwezo na nguvu hizo je Yule Aliyewaumba Atakuwa katika hali gani? Bila shaka Atakuwa juu zaidi.

Huruma na mapenzi ya Allah (Subhanahu Wataala) juu ya waja wake kwa kuwaekea viumbe wanaowahifadhi, kuwalinda na kuwasimamia. Kila mtu mmoja ana zaidi ya malaika ishirini waliomkalia mbele, nyuma, kuliani na kushotoni wanaomuhifadhi na kumsimamia kwa kumkinga na maafa mbali mbali yanayomkabili kila sehemu na kila wakati.

KUAMINI VITABU VYA ALLAH

Kuamini kuwa Allah (Subhanahu Wataala) Ameteremsha Vitabu kwa Mitume yake kama muongozo kwa waja wake na kwamba habari na maelezo yote yaliyomo katika vitabu hivyo ni kweli na hakuna shaka kuwa ni maneno ya kweli kutoka kwa Allah (Subhanahu Wataala).

Vitabu vilivyotajwa katika Qur'ani ni vinne (4) :

TAURATI- Allah (Subhanahu Wataala) Amemteremshia Nabii Musa (Alaihi Salaam).

ZABURI- Allah (Subhanahu Wataala) Amemteremshia Nabii Daud (Alaihi Salaam).

INJILI- Allah (Subhanahu Wataala) Amemteremshia Nabii Isa (Alaihi Salaam).

QUR'ANI- Allah (Subhanahu Wataala) Amemteremshia Nabii Muhammad (Swallallahu Alaihi Wasallam).

KUIAMINI QUR'ANI

QUR'ANI ni maneno ya Allah (Subhanahu Wataala) Aliyoyateremsha kwa Mtume wake Muhammad (Swallallahu Alaihi Wasallam) yaliyoandikwa katika misahafu na kufanywa kuwa ibada kuisoma kwake.

LUGHA YA QUR'ANI:

Qur'ani imeteremshwa kwa lugha ya kiarabu ili iwe

rahisi kwa watu wote kuifahamu. Allah (Subhanahu Wataala) Amesema:
"Hakika Sisi Tumeiteremsha hiyo Qur'ani kwa kiarabu (lugha fasaha iliyo bayana) ili mupate kuifahamu" Qur’ani [12:2].
Aya inafahamisha kuwa lugha ya kiarabu ndio lugha pekee inayoweza kueleza maana halisi ya Qur'ani yenye kutosheleza kwa uwazi na ufasaha, hivyo ili kunufaika na ujumbe wa Qur'ani, ni muhimu sana kufahamu misingi ya lugha ya kiarabu.

KUTEREMKA QUR'ANI:

Qur'ani imeteremka kwa awamu mbili (2) kuu:
1-Qur'ani imeteremka kwa ujumla kutoka katika LAUHUL MAHFOUDH [Ubao wa Allah (Subhanahu Wataala) uliohifadhiwa] mpaka katika BAITUL IZZAH [Nyumba tukufu ya Allah (Subhanahu Wataala) iliyopo katika mbingu ya dunia] katika usiku wenye cheo katika mwezi mtukufu wa Ramadhani.
2-Qur'ani imeteremka kutoka Baitul Izza mpaka kwa Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) kupitia malaika Jibril (Alaihi Salaam) kwa njia ya Wahyi kidogo kidogo kwa mujibu wa matokeo kwa muda wa miaka ishirini na tatu (23), miaka kumi na tatu (13) Qur'ani imemteremkia Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) akiwa Makka na miaka kumi (10) imeteremka akiwa Madina.

Katika kipindi cha Khalifa wa kwanza Abuubakar (Allah Amridhie) Qur'ani imekusanywa na kuwekwa katika mfumo wa kitabu. Katika kipindi cha Khalifa wa nne Aliy (Allah Amridhie) Qur'an ikatiwa irabu yaani fat-ha, kasra, dhumma na sukuni. Katika kipindi cha Abdulmalik Ibn Marwan Qur'ani ndio ikatiwa nukta ili kuzitofautisha herufi zake zilizofanana na hivyo ndivyo ilivyo mpaka hivi sasa. Qur'ani ina juzuu 30, sura 114 na aya 6236. Sura kubwa zaidi ni Surat Al-Bakara ambayo ina aya 286 na ndogo zaidi ni Surat Al-Kauthar ambayo ina aya tatu na maneno yasiyozidi 11. Sura bora kuliko zote ni Surat Al-Faatiha ambayo ndiyo sura ya mwanzo (Sura ya Utangulizi) katika Qur'ani kwa mpangilio wa Mus'haf na aya bora kuliko zote ni ayat Al-Kursiyyu iliyopo katika Surat Al-Bakara. Aya za mwanzo kuteremka ni aya tano za mwanzo za Surat Al- Alaq (Iqra) na aya ya mwisho kuteremka ni aya ya 281 ya Surat Al-Bakara.

Aya za Makka zinakuwa fupi fupi zenye miujiza ya maajabu ya uumbaji na utukufu wa Allah (Subhanahu Wataala) ili kuwajenga IMANI walengwa ili wafahamu kuwa yupo Muumba, Mmmiliki, Msimamiaji na Muendeshaji wa huu ulimwengu wakati aya na sura za Madina mara nyingi zinakuwa ndefu na zinawalenga watu wenye Imani ambao wako tayari kutekeleza amri zote na makatazo ya Allah (Subhanahu Wataala); Aya

zake mara nyingi zinaanza na “Enyi Mlioamini” na kubwa kuliko zote ni aya ya 282 ya Surat Al-Bakara inayoitwa “Ayat Ad-Dain” aya ya deni ambazo mara nyingi zinazungumzia maswala ya sheria, hukumu, amri na makatazo mbali mbali.

UBORA WA QUR'ANI:

Qur'ani ni maneno ya Allah (Subhanahu Wataala) na ubora wake juu ya maneno mengine ni kama ubora wa Allah (Subhanahu Wataala) kwa viumbe wake!

MIUJIZA YA QUR'ANI:

Kwa nini Qur'ani ni muujiza?

Qur'ani ni muujiza kwa sababu nyingi lakini kubwa zaidi ni kule kushindwa watu wote na majini kuleta mfano wa sura moja tu iliyofanana na Qur'ani!

Ikiwa na maana kwamba ni maneno ya kweli yanayotoka kwa Allah (Subhanahu Wataala).

Qur’ani tangu ilipoteremshwa mpaka sasa imebakia katika asili yake bila kupunguzwa au kuengezwa au kubadilishwa chochote na lau kama misahafu yote duniani itakusanywa na itachomwa moto basi msahafu wa mwisho hauwezi kuungua na kama utaungua basi baada ya masaa machache tu itaandikwa tena upya kama ilivyokuwa mwanzo kwa vile imehifadhiwa yote katika vifua vya mamia ya waislamu kote duniani.

Mpangilio, ufasaha na ukweli wa maneno ya Qur’ani unaendelea kuwashangaza na kuwasilimisha mamia ya watu duniani wakiwemo wataalamu na wanasayansi wa fani mbali mbali ambao wamethibitisha kuwa kweli ni maneno ya Allah (Subhanahu Wataala) Aliyomfunulia Mtume wake (Swallallahu Alaihi Wasallam) na hayawezi kuwa maneno ya binadamu kutokana na kutoa habari ya mambo ambayo mwanadamu hawezi kuyadiriki kutokana na upeo mdogo wa elimu yake.

Baadhi ya mambo machache katika mengi ya kisayansi ambayo Qur’ani imeyataja zamani zaidi ya karne kumi na tatu (13) nyuma na yamegunduliwa na wanasayansi na kuthibitishwa katika karne ya 19 na 20 ni pamoja na asili, chanzo na kupanuka kwa Ulimwengu (Qur’ani 21:30), asili, chanzo na hatua za kuumbwa mwanadamu katika fuko la uzazi (Qur’ani 23:12-14), Milima kuwa na sifa ya vishikilio vya ardhi (Qur’ani 78:7), Aina mbili tofauti za maji ya bahari kukaa pamoja bila ya kuchanganyika (Qur’ani 55:19-20), Uwepo wa nyuki wa kike wafanyao kazi kwa bidii ikapatikana asali safi yenye tiba (16:68-70), Kuzunguka katika orbits magimba ya angani, mwezi, dunia, jua na nyota bila kuingiliana (Qur’ani 36:38-40) na kadhalika. Yote hayo yametajwa katika Qur’ani katika kipindi ambacho hakuna maendeleo yoyote ya sayansi na tehama, darubini za angani na vipima anga kama ilivyo sasa.

FADHILA ZA QUR'ANI:

Katika ubora wa kujifunza na kuwafunza wengine Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema "Mbora wenu ni yule anayejifunza Qur'ani kisha akaifundisha kwa wengine" (Hadithi Sahihi).

Katika ubora wa kuisoma Qur'ani Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema "Mwenye kusoma herufi moja katika kitabu cha Allah (Subhanahu Wataala) hupata mema kumi na jema moja ni kwa kumi mfano wake" Yaani kila herufi moja unapata thawabu kumi hivyo ukisoma suratul Faatiha (Al-Hamdu) pekee unapata thawabu 1560, Yaani herufi 156 mara kumi.

KUIHAMA QUR'ANI:

Imekuja katika Qur'ani kuwa ‘‘Na Amesema Mjumbe wa Allah "Ewe Mola wangu! Hakika watu wangu wameifanya hii Qur'ani kuwa ni yenye kuhamwa" Qur’ani [25:30]

Nini maana ya kuihama Qur'ani?

Amesema Imam Ibn Taymiya (Allah Amrehemu) katika kufafanua maana ya kuihama Qur'ani "Yule asieisoma Qur'ani ameihama na mwenye kuisoma Qur'ani bila kuzingatia maana yake ameihama na yule mwenye kuisoma na akaizingatia maana yake bila kuifanyia kazi nae pia ameihama!"

Kwa ufupi kuihama Qur'ani ni kutoisoma, kutoisikiliza, kutoizingatia maana yake na kutoifanyia kazi.

Basi ndugu zangu tujihimizeni na tuwahimize wenzetu katika kutenga muda kila siku wa kuisoma au kuisikiliza Qur'ani wala isipite siku bila kusoma au kusikiliza chochote katika Qur'ani, tusiache kujizolea thawabu nyingi mno kwa urahisi kabla haijafika siku ambayo mtu atakuwa tayari kumtoa mtoto wake, mke wake, ndugu yake na watu wote ili apate thawabu moja tu ya kumuokoa na adhabu siku nzito ya kiyama.

Kupitia Qur’ani, Waumini wanapata matumaini, amani, msaada mkubwa na rehema ya Allah (Subhanahu Wataala) kwa kuwateremshia mawaidha, hoja, mazingatio na muongozo maalum utakaowafikisha salama kwa Mola wao.

KUAMINI MITUME

Maana yake kwa ujumla ni kuamini kuwa Allah (Subhanahu Wataala) Amewachagua na kuwatuma Mitume katika kila umma ili kuwalingania (kuwaita) watu wamuabudu Allah (Subhanahu Wataala) na waache kumshirikisha na kitu chochote. Mitume ni watu maalum wenye sifa maalum walioteuliwa na Allah (Subhanahu Wataala) kufikisha ujumbe wake kwa watu maalum waliomkanusha Allah (Subhanahu Wataala). Allah (Subhanahu Wataala) Ametuma zaidi ya Mitume (Anbiyaa/Annabiyyiin) laki moja, katika hao akawateuwa zaidi ya Mitume (Al-Mursaliin) mia tatu

wa mwanzo akiwa ni Nabii Nuh (Alaihi Salaam) na wa mwisho ni Muhammad (Swallallahu Alaihi Wasallam). Pia wapo Mitume watano wanaoitwa *Ulul-Azmi (Wenye Azma yaani waliochukua ahadi nzito ya kufikisha ujumbe wa Allah Subhanahu Wataala)* ambao ni Nuh, Ibrahim, Musa, Isa na Muhammad.

Mitume waliotajwa katika Qur'ani ni 25:

- **Adam** – Baba wa wanadamu, aliumbwa kwa udongo na kuanza historia ya mwanadamu.
- **Idris** – Mtume mwenye elimu, uvumilivu na aliinuliwa daraja na Allah.
- **Nuh** – Mtume wa umri mrefu, Alihubiri tauhidi kwa watu wake.
- **Hud** – Alitumwa kuwaonya watu wa 'Aad waliokuwa na kiburi.
- **Swaleh** – Alipewa muujiza wa ngamia kuwa dalili kwa watu wa Thamud.
- **Ibrahim** – Rafiki wa Allah, shujaa wa tauhidi na baba wa mitume wengi.
- **Lut** – Aliwaonya watu wake dhidi ya maovu na machafu.
- **Ismail** – Mtume mtii, mwana wa Ibrahim, mshiriki wa ujenzi wa Kaaba.
- **Ishaq** – Mtume mwema, mwana wa Ibrahim na baba wa Yaqub.
- **Yaqub** – Mtume mwenye subira, baba wa makabila ya Israeli.

- **Yusuf** – Mtume wa subira na hekima, kisa chake ni kizuri katika Qur’ani.
- **Shuayb** – Mtume wa haki, alikemea udanganyifu katika biashara.
- **Ayyub** – Mtume wa subira kuu katika maradhi na mitihani.
- **Dhul-Kifl** – Mtume mwadilifu, mwenye kusimamia ahadi na haki.
- **Musa** – Mtume mkubwa, alitumwa kumkabili Firauni dhalimu.
- **Harun** – Mtume msaidizi, ndugu wa Musa katika daa wah.
- **Dawud** – Mtume na mfalme, alipewa Zaburi na sauti nzuri.
- **Sulayman** – Mtume na mfalme, alitawala majini, upepo na wanyama.
- **Ilyas** – Mtume aliyepambana na ibada ya masanamu.
- **Al-Yasa ‘**– Mtume aliyeendeleza ujumbe wa Ilyas kwa watu wake.
- **Yunus** – Mtume wa toba, aliokolewa baada ya kumezwa na samaki.
- **Zakariya** – Mtume mcha Mungu, alimuomba Allah mtoto kwa subira.
- **Yahya** – Mtume safi na mchamungu, aliuliwa shahidi.
- **Isa** – Mtume wa Injili, alizaliwa bila baba kwa muujiza.
- **Muhammad** ﷺ – Mtume wa mwisho, rehema kwa walimwengu wote.

UTUME WA NABII MUHAMMAD

Mtume wetu Muhammad ﷺ ndiye Mtume wa mwisho Aliyetumwa kwa Umma wa mwisho na kuteremshiwa ujumbe wa Mwisho (Qur'ani).

Ni muhimu sana kufahamu japo kwa ufupi sana historia yake kutoka katika vitabu sahihi vilivyoeleza Maisha ya Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam).

Vitabu marufu na sahihi vilivyoeleza maisha ya Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) ni pamoja na Sira ya Ibn Hisham, Sira ya Ibn Kathir, Zaad Al-Maad cha Imaam ibn Qayyim Al-Jauziyy, Siyari Aalaamin Nubalaa cha Imaam Ad-Dhahabiy, Allu'ulu'ul Maqnuun cha Sheikh Musa Al-Azimiyy, Nuurul Yaqeen cha Sheikh Muhammad Al-Khudhariyy n.k.

MAISHA YA NABII MUHAMMAD

Jina lake ni Muhammad mtoto wa Abdullah ambae ni mtoto wa Abdulmuttalib mtoto wa Hashim wa kabila tukufu la kikuraish na ***mama yake*** anaitwa Aaminah mtoto wa Wahab ambae ni mtoto wa Abdumanaaf mtoto wa Zuhrah. Nasabu yake imeishia kwa bwana Adnan ambae ni mmoja katika wajukuu wa Nabii Ismail (Alaihi Salaam) mtoto wa Nabii Ibrahim.

Amezaliwa katika mji mtukufu wa MAKKA katika alfajiri ya Jumatatu, mwezi wa mfunguo sita (Rabiul Awwal) mwaka wa tembo (mwaka lilioangamizwa jeshi

la Abraha kutoka Yemen aliyetaka kuivunja Al-kaaba akiwemo tembo mkubwa aliyeitwa mahmoud) sawa na tarehe 20 August 570 B.I.

Baba yake amekufa kabla hajazaliwa na mama yake amekufa alipotimia umri wa miaka sita (6) Akalelewa na ***Babu yake*** Bwana Abdulmuttalib na Alipotimia umri wa miaka 8 babu yake nae akafariki Akalelewa na Ami yake bwana Abuu Talib.

Katika ***utoto wake*** Amechunga mbuzi kama ilivyo kwa Mitume wenzake (wote) waliomtangulia na hekima ya Mitume wote kuchunga mbuzi au kondoo kabla kupewa utume ipo wazi lakini kwa ufupi ni kuwa Mitume walipata mafunzo mbalimbali katika kuchunga wanyama ili iwe rahisi kuwachunga na kuwasimamia wanadamu, miongoni mwa mafunzo hayo ni subra (uvumilivu), upole, ushujaa na unyenyekevu.

Alipotimia umri wa miaka tisa (9) Alisafiri pamoja na ***Ami yake*** katika msafara wa kibiashara kuelekea Sham (Syria) kwa mara ya kwanza lakini njiani wakakutana na Mwanachuoni mmoja wa kinaswara, baada tu ya kumuona alimtambua kwa alama kadhaa kuwa ndiye huyo Mtume anayesubiriwa aliyebashiriwa katika Taurati na Injili hivyo haraka akamwambia Bwana Abu Talib arejee naye Makka ili Mayahudi wasimtambue ikawa sababu ya kumdhuru hivyo Bwana Abu Talib akarejea naye Makka.

Alipotimia ***umri wa miaka 25***, Alisafiri kuelekea Shaam (Syria) mara hii akiwa ni mfanya biashara wa mwanamke tajiri na mtukufu katik mji wa Makka Bi ***Khadija*** mtoto wa Khuwailid, na baada ya kurejea baada ya miezi miwili Alimtaka amuoe baada kushangazwa na ukweli na uaminifu wake kwa hivyo akamuoa na Allah (Subhanahu Wataala) Akamruzuku kutokana naye watoto sita, wanne wanawake na wawili wanaume.

Bibi Khadija alikuwa na umri wa miaka 40 alipoolewa na Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) na wameishi pamoja kwa muda wa miaka 25.

Alikuwa anapenda ***kukaa peke yake*** na kuwafikiria watu wake ambao walikuwa wanaabudu masanamu, wakati huo alikuwa tayari ameshajulikana na kuenea kwa sifa nzuri na kuwa mbali na desturi za ujinga mpaka watu wake wakamwita "mkweli muaminifu".

Katika muda huu Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) alikuwa akifuata na kuabudu mila/dini ya babu yake (Nabii Ibrahim Alaihi Salaam).

KUANZA WAHYI (UTUME):

Alipotimia umri wa ***miaka 40*** ulimjia wahyi (utume) kupitia malaika Jibril akiwa katika pango la Hira, hivyo aya tano za mwanzo za Surat Al-Alaq zikateremka katika mwezi mtukufu wa Ramadhani sawa na 610 B.I. Akakaa katika mji wa Makka kwa muda wa miaka 13

akiwalingania watu wake kwa njia tofauti ili wamtambue Mola wao.
Katika muda huu Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Alikabiliana na ***changamoto*** mbali mbali kutoka kwa Makureish baada tu ya kudhihirisha wito wake wa kumuabudu Mola mmoja! hivyo walimbadilikia wakawa wanamuudhi na kuwaudhi wafuasi wake ambao bado walikuwa wachache sana, hali ilipokuwa ngumu aliwaamuru wakatake himaya katika nchi ya Uhabeshi (Ethiopia) ambapo kipindi hicho ilikuwa chini ya ***Mfalme Najashi*** aliyeitwa Aswhama ibn Abhar, huyu alikuwa haruhusu mtu yeyote kudhulumiwa katik nchi (mamlaka) yake.
Waislamu walianza kupata matumaini kidogo baada ya kusilimu Hamza na baadae Umar (Allah Awaridhie) wakawa wanadhihirisha ibada zao.
Katika mwaka wa 10 B.U-***Mwaka wa huzuni***, Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) alifiwa na mkewe Bi Khadija (Allah Amridhie) na Ami yake Bwana Abuu Talib ambao walikuwa watu muhimu sana katika maisha yake ya Utume katika mji wa Makka.
Baadae Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) alikwenda ***Twaif*** kisha baada kurejea bila mafanikio katika usiku wa Jumatatu mwezi 27 Rajab 11 B.U sawa na 621 B.I, Alipokea mualiko wa safari tukufu ya Isra (kutoka Masjid Al-Haraam-Makka mpaka Masjid Al-

Aqswa-Palestine) na Miiraaj (kutoka Masjid Al-Aqswa mpaka Mbingu ya 7) ambako huko alifaradhishiwa swala tano kama zawadi kwa Umma wake.

KUHAMIA MADINA:

Katika siku ya Jumatatu mwezi 12 mfunguo sita mwaka wa 13 wa utume wake sawa na tarehe 28 June 622 B.I Alihamia katika mji wa YATHRIB na akakaa hapo kwa muda wa miaka kumi (10).

Mji wa ***Yathrib*** kuanzia hapo ukawa unajulikana kama mji wa MADINA (MJI WA MTUME) na ukawa mwaka aliohama Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) kutoka Makka kuja Madina ndio kuanza kwa tarekhe mpya ya kiislamu na mtu wa mwanzo aliyeanzisha tarekhe ya kiislamu ni Khalifa wa pili Umar (Allah Amridhie) katika ukhalifa wake.

Waislamu hawakuwa kama umma wa kiislamu katika mji wa makka kwa sababu walikuwa wachache na wasio na nguvu na ndio maana Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) hakuamrishwa kujihami kwa kupigana bali aliamrishwa kusubiri maudhi aliyokuwa akifanyiwa na maadui zake.

Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) alipofika na kutulia katika mji wa Madina alianza kueka misingi madhubuti kwa ajili ya umma bora wa kiislamu ambao haujawahi kushuhudiwa katika historia ya ulimwengu.

Miongoni mwa misingi hiyo muhimu ni:

1- ***Kujenga Mskiti wa Madina*** uliokuwa kituo muhimu katika harakati za uislamu, waislamu walikuwa wanautumia mskiti huu kwa ajili ya ibada, taalimu, kuhukumiana na mahafali mbali mbali yaliyojenga ukaribu mkubwa baina yao.
2- ***Kuwaunganisha*** MUHAJIRINA (waliotoka Makka pamoja na Mtume) na ANSWAAR (wenyeji wa Madina waliompokea ambao wamegawanyika makabila makuu mawili ya kiudugu ya AUS na KHAZRAJ ambao pia Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) aliwaunganisha baada kuwa ni maadui wao kwa wao) wote wakawa ndugu na wamoja katika dini baada ya kuwa wamoja katika makabila yao.
3- ***Mikataba*** ya kusaidiana baina ya waislamu na wasiokuwa waislamu ambao wamegawanyika makundi mawili makuu: waarabu na mayahudi (Banu Nadhir, Banu Quraidha na Banu Qainuqaa ni makabila makuu ya mayahudi waliokuwepo katika mji wa Madina ambao daima walikuwa wakiwafitinisha Aus na Khazraj wakawa hawaachi kupigana wao kwa wao).
4- ***Misingi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii*** kwa sababu Uislamu ni Dini na Dola vile vile kwa hivyo kukawa na umuhimu mkubwa wa kueka misingi hii. Hivyo aya nyingi zilizoteremka Madina zilikuwa zinalenga katika kueka sheria za misingi hii.
Kwa namna hii Aliweza Mtume (Swallallahu Alaihi

Wasallam) kuanzisha jamii ya kwanza ya kiislamu iliyoishi maisha bora iliyoshikamana katika pande zote, wote wakiwa ndugu na usawa uliotanda katika jamii nzima.

Baada ya hapo Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) na wafuasi (Maswahaba) wake (Allah Awaridhie) walipokea sheria za amri mbali mbali kutoka kwa Allah (Subhanahu Wataala) kama vile Jihadi, Funga ya Ramadhani, Zaka, Hija, Hijabu, Swala za Iddi n.k.

Vita vikubwa katika maisha ya Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) ni:

1- ***BADRI***: Mwezi 17 Ramadhani mwaka wa 2 B.H sawa na January 624 B.I. Waislamu walikuwa 313 wakiwa na vifaa na silaha dhaifu na Makafiri wa kikuraish wakiwa 1,000 wakiwa na vifaa na silaha za kutosha. Waislamu walishinda kwa msaada mkubwa wa Allah Subhanahu Wataala.

2- ***UHUDI***: Shawwaal mwaka wa 3 B.H sawa na January 625 B.I. Waislamu walikuwa takriban 700 huku makuraishi wakiwa 3,000. Waislamu walishindwa lakini walijifunza utiifu na subira.

3- ***KHANDAQ (AHZAAB)***: Shawwaal mwaka wa 5 B.H sawa na February 627 B.I. Makafiri waliungana dhidi ya waislamu lakini Allah Subhanahu Wataala

Aliwanusuru Waislamu kwa upepo na Malaika, makafiri wakakimbia kwa khofu na khasara kubwa.

4- ***KHAIBAR***: Muharram mwaka wa 7 B.H sawa na August 628 B.I. Waislamu walishinda baada ya kuvunja ngome za mayahudi waliovunja mikataba waliyoekeana na Mtume Swallallahu Alaihi Wasallam.

5- ***FAT-HU MAKKAH***: Ramadhani mwaka wa 8 B.H sawa na January 630 B.I. Mji wa Makka ukakombolewa, masanamu yakavunjwa, ushirikina ukaondolewa na watu wengi wakaingia katika Uislamu bila kulazimishwa makundi kwa makundi.

6- ***HUNAIN***: Mwezi 10 Shawwaal mwaka wa 8 B.H sawa na February 630 B.I. Baada ya kukombolewa mji wa Makka, vita vya Hunain vikafuata ambapo Waislamu walipata upinzani mkali wasioutarajia mwanzoni lakini baadae Allah Subhanahu Wataala aliwapa utulivu wakapata ushindi mkubwa dhidi ya makabila ya Hawazin na Thaqif.

7- ***TABUUK***: Rajab mwaka wa 9 B.H sawa na October 630 B.I. Vita vya Tabuuk vilitokea dhidi ya Warumi. Havikuwa na mapigano makubwa lakini ni safari ngumu iliyothibitisha subira na utiifu mkubwa. Safari hii ya mbali pia ilithibitisha nguvu na umoja wa waislamu waliungana kwa udugu wa imani zao.

Allah Subhanahu Wataala Akautimiza Uislamu kama

ilivyokuja katika Qur'ani, Allah (Subhanahu Wataala) Amesema "...Leo nimeshawakamilishia Dini yenu (Dini ya Uislamu, kwa kuuhakikishia ushindi na kuikamilisha sheria) na nimewatimizia neema zangu kwenu (kwa kuwatoa kwenye giza la ujinga na kuwapeleka kwenye mwangaza wa imani) na nimewaridhia kwamba Uislamu ndio Dini, (basi shikamaneni nayo wala musiiache)..." Qur’ani [5:3].

Hivyo kabla kufariki Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Uislamu ulikuwa tayari umekamilika na kuenea pande zote za bara Arabu.

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema "Utakapokujia Ewe Muhammad ushindi kutoka kwa Allah (Subhanahu Wataala) na ukaufungua (ukaukomboa) mji wa Makka na ukaona watu wengi wanaingia katika dini ya Allah makundi kwa makundi, basi jitayarishe kukutana na Mola wako kwa kumtakasa na kumhimidi na kumuomba msamaha kwa wingi kwani Yeye ni mwingi wa kupokea toba" Qur’ani [110:1-3].

KUFARIKI DUNIA

Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) alifariki (kwa maradhi) mchana wa siku ya Jumatatu, mwezi 12 katika mwezi wa mfunguo sita mwaka wa 11 B.H sawa na tarehe 7 June 632 B.I Akiwa na umri wa miaka sitini na tatu (63).

Siku aliyokufa Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam)

ilikuwa siku mzito mno kwa Waislamu, Abuubakar (Swahaba anayependeza zaidi kwa Mtume na Khalifa wa kwanza baada yake) Alikuwa hayupo, Umar (Khalifa wa pili) alitoa upanga wake na kumtishia yeyote atakaesema kuwa Mtume Amefariki pamoja na kuwa Yeye vile vile amesikia khutba ya Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) kabla kufa kwake inayosema: "Enyi watu! Imenifikia kuwa nyinyi munaogopa mauti ya Mtume wenu ! Hebu niambieni amekaa milele kabla yangu Mtume yeyote ? Tambueni kuwa Mimi nitakutana na Mola wangu". Abuubakar alipopata khabari akaingia ndani akaufunua uso Mtukufu wa Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) kisha akaubusu huku akilia kisha akatoka nje akawatangazia watu baada kumsifu na kumshukuru Allah (Subhanahu Wataala) "Enyi watu yule ambae alikuwa akimuabudu Muhammad basi atambue kuwa Muhammad ameshakufa na yule ambae anamuabudu Allah basi Allah Yuko hai na hafi" Akasoma na baadhi ya aya za Qur'ani hapo ndio watu wakapata uhakika kuwa Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) kweli Amefariki dunia.

Muhimu:

B.I = Baada ya Nabii Isa, B.U = Baada ya Utume

B.H = Baada ya Hijra

KUAMINI SIKU YA MWISHO

Maana yake ni kuamini kila Alichoeleza Allah Subhanahu Wataala na Mtume wake (Swallallahu Alaihi Wasallam) katika yale yatakayotokea baada ya mauti. Katika mambo hayo ya ghaib ni haya yafuatayo :

FITNA ZA KABURINI NA MASWALI YA MALAIKA WAWILI (MUNKAR NA NAKIR)

Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema :

Anapoingizwa Mja kaburini huwa anasikia milio ya viatu vyao wanapoondoka, humjia Malaika wawili wakamkalisha kitako kisha humuuliza; Nani Mola wako? Atajibu; Mola wangu ni Allah Subhanahu wataala, Watamuuliza; ni ipi Dini yako? Atajibu; Dini yangu ni Uislamu, kisha Watamuuliza; Ni nani Mtu huyu Aliyetumwa kwenu? Atajibu; Yeye ni Mjumbe wa Allah Subhanahu Wataala. Ataambiwa; Angalia sehemu yako katika Moto, Allah Subhanahu Wataala Amekubadilishia sehemu nyengine katika sahemu za Peponi (Ataziona sehemu zote mbili)" (Hadithi Sahihi) Huyu bila shaka atakuwa ni Muumini, na katika Hadithi nyengine Mtume Swallahu Alaihi Wasallam Ameeleza "Ama Kafiri au Mnafiki Atasema; Sijui, nilikuwa nikisema juu ya Mtu huyu (yaani Mtume Swallallahu Alaihi Wasallam) vile walivyokuwa wakisema watu.

Ataambiwa; Hukujua wala hukusoma, kisha atapigwa rungu la chuma baina ya masikio yake, mpigo mmoja, atapiga kelele watasikia walio karibu yake isipokuwa watu na majini” [Hadithi Sahihi].

ADHABU NA NEEMA ZA KABURINI

Amesema Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) :

‘‘Hakika mmoja wenu anapokufa, huonyeshwa makaazi (mafikio) yake asubuhi na jioni, ikiwa ni katika watu wa peponi basi ni katika makaazi (mafikio) ya watu wa peponi na ikiwa ni katika watu wa motoni basi ni katika makaazi ya watu wa peponi, Ataambiwa Haya ndio makaazi yako mpaka utakapofufuliwa siku ya kiyama’’ (Hadithi Sahihi, Bukhari na Muslim)

DALILI ZA KIYAMA

Ni wajibu wa kila Muislamu kuamini kuwa kiyama kinakuja wala hakina shaka na hakuna anayejua kitatokea lini isipokuwa Allah (Subhanahu Wataala)

Katika dalili ndogo ndogo za kiyama zilizotajwa katika baadhi ya hadithi sahihi za Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) ni kikithiri matetemeko ya ardhi, kukaribiana kwa zama (muda) yaani mwaka kuwa kama mwezi, mwezi kuwa kama wiki, wiki kuwa kama siku na siku kuwa kama saa, kudhihiri fitna nyingi, kukithiri vifo, kushindana watu katika kurefusha majumba, kupotea

kwa amana yaani watu kupewa majukumu yasiokuwa yao, elimu kupotea, ujinga kudhihiri, kutangazwa maasi ya zinaa, pombe na kamari, wanawake kuwa wengi na wanaume kupungua, waislamu kupigana na mayahudi na nyenginezo nyingi.

Katika dalili kubwa za kiyama ni kuchomoza jua kutoka magharibi, kutoka mnyama ardhini, kudhihiri Masihi Dajjal (Mfitinishaji Mkuu), kushuka Nabii Isa Alaihi Salaam, kudhihiri Ya'ajuju na Ma'ajuju na nyenginezo nyingi.

KUANZA SIKU YA KIYAMA

Ni wajibu kuamini yale Aliyoyatolea habari Allah Subhanahu Wataala katika kitabu chake kitukufu Quran kuhusiana na matukio ya kuangamia kwa dunia na vyote vilivyomo khasa katika Surat At-Takwir, Surat Al-Infitwaar, Surat Al-Inshiqaaq, Surat Al-Qaariah n.k.

KUFUFULIWA VIUMBE

Baada ya kupulizwa parapanda au baragumu la kwanza la kufisha viumbe litapulizwa la pili la kufufua viumbe vyote wa mwanzo na wa mwisho na wa mwanzo kufufuka ni Mtume wetu Muhammad Swallallahu Alaihi Wasallam.

KUKUSANYWA VIUMBE

Kisha watakusanywa viumbe wote kwa ajili ya kuhesabiwa na kulipwa kila mmoja kile alichofanya akiwa duniani.

Watatoka katika makaburi bila viatu na nguo, watawaona kwa macho majini na malaika kila mmoja atakuwa na jambo lenye kumshughulisha yeye mwenyewe hatokuwa na nafasi ya kumfikiria mtu mwengine yeyote hata ndugu au mama au baba au mke au watoto wake.

KUAMINI PEPO

Allah Subhanahu Wataala Amesema :

‘‘Na kimbilieni kwenye msamaha utokao kwa Mola wenu na Pepo ambayo upana wake ni mbingu saba na ardhi, imeandaliwa kwa ajili ya Wachamungu (waumini wa kweli wanaotekeleza maamrisho na kuacha makatazo ya Allah Subhanahu Wataala)’’ Qur’ani, Surat Aal-Imran [3 :133].

Pepo ndio nyumba ya amani Aliyoiandaa Allah (Subhanahu Wataala) kwa ajili ya Wachamungu au Waumini wa kweli wanaume na Wanawake.

Wa mwanzo Atakayeingia katika Pepo ni Mtume wetu Muhammad (Swallallahu Alaihi Wasallam) na mtu wa

chini kabisa katika watu wa peponi ni yule atakayekuwa na mfano wa dunia nzima na vyote vilivyomo mara kumi na atahisi yeye ndiye mtu mwenye neema zaidi katika watu wote wa peponi !

Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema katika yale Aliyoyapokea kutoka kwa Mola wake kuhusiana na starehe za peponi kuwa Allah Amesema :

‘‘Nimewaandalia waja wangu wema yale ambayo jicho lolote halijawahi ona wala sikio lolote halijawahi sikia wala hayajawahi kupita katika moyo wa mtu yeyote’’.

Katika Pepo hakuna huzuni, magonjwa, kufa, kuumwa, kuzaa, kuchoka, kwenda haja, maneno mabaya na mambo yote yenye kuudhi na kukera yaliyopo duniani.

Pepo ina daraja mbalimbali kulingana na imani na matendo ya waja na daraja ya juu kabisa ni Firdaus.

Qur’ani inaeleza kuwa katika pepo kutakuwa na mito ya maji safi matamu, mito ya maziwa, mito ya asali na mito ya mvinyo isio na madhara kwa mnywaji.

Qur’ani pia imeeleza kuwa katika pepo kutakuwa na wanawake (Hoorul-Ayn) watakaokuwa na uzuri wa ajabu, wenye macho makubwa yenye mboni nyeupe safi, wenye upendo na umri wa ujana wa kudumu.

Imeelezwa pia kuwa waumini wanawake wa duniani katika pepo watakuwa wazuri zaidi kuliko hao mahoorul-ayn kwa sababu ya imani zao na matendo yao mema waliyoyafanya duniani. Mwanamke mwema wa duniani ataungana na mume wake mwema wa duniani ikiwa wote walikuwa waumini wataishi pamoja milele.

Pepo si mahali pa kutosheleza matamanio ya kimwili tu peke yake bali ni makazi ya furaha ya milele yaliyoridhiwa na ukamilifu wa neema.

Ladha za peponi za kula, kunywa, kujimai na kadhalika ni zenye kudumu hazikatiki au kukinaisha kama ladha za duniani.

Tunamuomba Allah (Subhanahu Wataala) kwa rehema Yake Atuingize katika watu wa Peponi Aamin.

KUAMINI MOTO

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema :

‘‘Enyi Mlioamini (Wenye kumuamini Allah na Mtume wake) ziokoeni nafsi zenu (kwa kutekeleza maamrisho na kuacha makatazo) na nafsi za jamaa zenu na moto ambao kuni zake ni watu na mawe. Juu ya moto huo wapo Malaika (Zabaniya) wakali wenye nguvu (walio thabiti katika usimamizi wao), Hawamuasi Allah Subhanahu Wataala na wanafanya yote wanayoamrishwa (bila kuchoka)’’ Qur’ani (66 :6)

Moto ndio makaazi Aliyoyaandaa Allah Subhanahu Wataala kwa Makafiri, Wanafiki, Washirikina na wote wanaomuasi Allah Subhanahu Wataala bila kutubia.

Moto wa Jahannam ni mkali kuliko moto wa duniani kwa mara sabini (70), wenye giza na wenye kusimamiwa na malaika (Zabaniyah) wenye ukali na wasio na huruma kwa wakazi wake.

Mtu atakayepata adhabu ya chini zaidi katika watu wa motoni ni mtu Atakayeekewa makaa mawili ya moto wa Jahannam chini ya nyayo zake na ubongo wake utachemka na atahisi hakuna mtu yeyote aliyepewa adhabu kubwa zaidi kuliko yeye katika watu wote wa motoni.

Tunamuomba Allah Subhanahu Wataala Atukinge na Adhabu ya Moto Aamin.

KUAMINI QADAR

Maana yake ni kuamini kuwa yote yaliyotokea, yanayotokea na yatakayotokea yameshapangwa kuwa yatatokea kwa makadirio maalum na matakwa yake Allah (Subhanahu Wataala) kwa hekima maalum Anayoijuwa Yeye peke yake. Mtume Swallallahu Alaihi Wasallam Amesema ‘Ameandika Allah Subhanahu Wataala makadirio (mipango) ya viumbe vyote kabla hajaumba mbingu na ardhi kwa miaka elfu

khamsini’ (Hadithi Sahihi) Pia Amesema ‘Kila kinachotokea kinatokea kwa Qadar’ yaani hakitokei tu bila sababu au mpango maana yake ni kuwa halianguki hata jani lolote katika mti wowote isipokuwa linaanguka kwa hesabu, amri na matakwa yake Allah Subhanahu Wataala. Analotaka Yeye Allah Subhanahu wataala huwa na asilolitaka haliwi, Anajua yote yaliyotokea, yote yanayotokea, yote yatakayotokea na yote yasiyotokea kama yangetokea yangetokea vipi. Elimu yake imekienea kila kitu katika Ulimwengu.

SIFA ZA WAUMINI

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema :

‘‘Hakika (Si vyenginevyo) Waumini (wa kweli) ni wale ambao Akitajwa Allah (Subhanahu Wataala) nyoyo zao zinaingiwa na hofu, wasomewapo aya za Allah (Subhanahu Wataala) zinawazidishia Imani (pamoja na imani waliyonayo) na kwa Mola wao wanategemea (hawamtarajii na hawamuogopi yeyote isipokuwa Allah Subhanahu Wataala)**,** Wale ambao wanasimamisha swala (wanaswali swala tano kwa kuchunga sharti na nguzo zake kwa unyenyekevu) na katika kile tulichowaruzuku wanatoa (kwenye yale tuliyowaamrisha katika zaka na swadaka), Hawa (wenye sifa hizi) ndio Waumini wa kweli, watakuwa na

daraja za juu mbele ya Mola wao, msamaha wa dhambi zao na riziki nzuri (yaani pepo)’’. Qur’ani, [8 :2-4].

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema :

‘‘Kwa hakika wamefaulu Waumini, wale ambao (miongoni mwa sifa zao) ni wanyenyekevu katika swala zao, na wale ambao mambo ya upuuzi wanayapuuza, na wale ambao wanatoa zaka, na wale ambao wanazihifadhi tupu zao (kutokana na uzinifu, ulawiti na machafu mengine) isipkuwa kwa wake zao au wajakazi waliomilikiwa na mikono yao ya kulia, kwao hao hawana lawama [wala makosa kuwaingilia na kustarehe nao kwa kuwa Allah (Subhanahu Wataala) Amewahalalishia], basi mwenye kutafuta kujistarehesha kwa wasiokuwa hao, basi hao watakuwa ni wenye kuchupa mipaka waliyohalalishiwa na kuingia katika mambo ya haramu yenye kuwaingiza katika mateso na hasira za Allah (Subhanahu Wataala). Na (Waumini) ni wale ambao wanazichunga amana na ahadi zao na wale ambao wanazihifadhi swala zao (kwa kuzidumisha na kuzitekeleza kwa wakati wake kwa sharti zake na nguzo zake). Hao (wenye sifa hizo) ndio warithi. Ambao watairithi pepo ya juu kabisa (Firdaus) watakaa humo milele (hazitakwisha na kukatika neema zao)’’.

Qur’ani, Surat Al-Muminuun [23 :1-11].

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema :

‘‘Hakika (si vyenginevyo) Waumini (wa kweli) ni wale waliomuamini Allah (Subhanahu Wataala) na Mtume wake kisha wasiwe na shaka katika imani yao, na wakafanya juhudi kwa kutoa mali zao na nafsi (roho) zao kwa kupigana katika njia ya Allah (Subahahu Wataala), basi hao (wenye sifa hizo) ndio wakweli (katika imani yao)’’ Qur’ani, Surat Al-Hujurat [49 :15].

NAFASI YA SWALA KATIKA UISLAMU

Swala katika Uislamu si ibada ya kawaida tu – ni nguzo kuu, kipimo cha imani, na kitambulisho cha muumini. Wanazuoni wameipa nafasi ya kipekee sana kwa kuizingatia Qur’ani, Hadithi na athari za Maswahaba.

1. Swala ni Nguzo ya Pili ya Uislamu

Mtume ﷺ Amesema:

> “Uislamu umejengwa juu ya mambo matano: Shahada… na kusimamisha Swala …” (Bukhari & Muslim)

Hii inaonesha kuwa:

Bila Swala, “jengo” la Uislamu wa mtu linatetereka au huanguka.

Ni baada ya Shahada tu ndipo Swala hufuata.

📌 Hii inaipa Swala nafasi ya pili katika dini nzima

2. Swala ndiyo Tofauti kati ya Muumini na Kafiri

Mtume ﷺ Amesema:

> “Hakika tofauti kati ya mtu na shirk/kufuru ni kuacha Swala.” (Muslim)

Wanazuoni wengi wamesema:

Aliyeacha Swala kwa makusudi yuko katika hatari kubwa ya kukufuru!

Swala ndiyo alama ya wazi ya Imani

📌 Swala ni mpaka kati ya: ✅ Imani na ❌ Ukafiri

3. Swala ndiyo Ibada Pekee Iliyoamrishwa Mbinguni

Swala haikuteremshwa kwa Mtume akiwa duniani

kupitia Malaika akiwa ardhini bali iliamrishwa usiku wa Israa na Mi'raaj, Mtume ﷺ Alipanda mpaka mbingu ya saba.

📌 Hii inaonesha:

Ni ibada yenye heshima ya juu zaidi.

Allah alizungumza na Mtume moja kwa moja kuhusu swala.

4. Swala ni Alama ya Kuzungumza na Allah

Mtume ﷺ Amesema:

> “Mmoja wenu anaposwali, huwa ananong’ona na

Mola wake...” (Bukhari)

Maana yake:

Swala ni mazungumzo (mawasiliano) ya moja kwa moja kati ya mja na Mola wake

Unaposema “Alhamdulillah…” Allah naye hujibu “Amenihimidi (Amenisifu na kunishukuru) Mja wangu”

📌 Ni ibada ya karibu sana kiroho

5. Swala Inazuia Maovu na Machafu

Qur’an inasema:

> “Hakika Swala humzuia mtu na mambo machafu na maovu.” (29:45)

Hapa wanazuoni wanasema:

Kadri swala inavyokuwa sahihi, ndivyo tabia za muumini zinavyonyoka

Swala hufanya moyo uwe safi

📌 Swala ni “ngome ya kimaadili”

6. Swala ni Kipimo cha Imani ya Mtu

Sio kila mtu anayeswali yuko sawa:

Wapo wanaoswali kwa ada tu

Wapo wanaoswali kwa ikhlasi na khushuu

Mtume ﷺ Amesema:

> “Kuna mtu ataswali na hataandikiwa chochote ila

robo, nusu, au ndogo zaidi...” (Ahmad)

📌 Ubora wa swala = nguvu ya imani

7. Swala ni Jambo la Kwanza Kuulizwa Siku ya Kiyama

Mtume ﷺ Amesema:

> “Jambo la kwanza atakaloulizwa mja Siku ya Kiyama ni Swala yake.” (Tirmidhy)

Ikiwa Swala itakuwa sawa: ➡ Matendo mengine yataangaliwa kwa urahisi

Ikiwa Swala itaharibika: ➡ Mengine pia yataharibika

📌 Swala ni kipimo cha mwisho cha mafanikio

8. Swala ni Nuru kwa Muumini

Mtume ﷺ Amesema:

> “Swala ni nuru...” (Muslim)

Maana:

Nuru duniani (mwongozo)

Nuru kaburini na nuru Siku ya Kiyama

Wenye kuilinda Swala:

✅ Nyuso zao hutanuka ✅ Moyo wao hutulia

9. Swala Humjengea Muumini Nidhamu ya Maisha

Katika swala unajifunza:

Kuchunga muda (punctuality)

Usafi (twahara)

Nidhamu (safu)

Heshima (qibla)

Subira (kusubiri iqama)

📌 **Swala = shule ya maadili**

10. Swala Inamletea Mtu Rehema za Allah

Swala inafungua mlango wa baraka, rehema na maghfirah (msamaha).

Wanazuoni wamesema:

> “Yule anayesimamisha Swala yake — amesimamisha dini yake.

Na yule anayeiacha Swala yake — ameivunja dini yake.”

Kwa ufupi (muhtasari):

1. **Swala ni nguzo ya dini**
2. **Ni tofauti ya muumini na kafiri**
3. **Ni mazungumzo (mawasiliano) na Allah**
4. **Inasafisha tabia**
5. **Ni jambo la kwanza kuulizwa siku ya kiyama**
6. **Ni nuru ya maisha**
7. **Ni kipimo cha imani**
8. **Inaleta rehema na baraka**

9. Ni kinga dhidi ya madhambi

10. Ni njia ya Pepo

MAMBO YA IMANI

Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Ameeleza sehemu, alama, vipimo na mambo ya Imani katika baadhi ya Hadithi Sahihi zifuatazo :

Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema:

"Imani ni zaidi ya sehemu sabiini (70) ya juu zaidi ni LAA ILAAHA ILLALLAH na ya chini zaidi ni kuondosha udhia (mfano wa mwiba) katika njia na HAYA ni sehemu katika imani" [Hadithi Sahihi].

Uchambuzi:

Wanazuoni wa Ahlus-Sunnah, khususan Imam Al-Bayhaqi kwenye kitabu chake Shu‘abul Iman, pamoja na wanazuoni kama An-Nawawi, Ibn Hajar, Al-Qurtubi na wengine, wameeleza vipengele hivi vya imani katika makundi makuu matatu:

A - Matawi ya Imani ya Moyo (itikadi)

B - Matawi ya Imani ya Ulimi (kauli)

C - Matawi ya Imani ya Vitendo (matendo ya viungo)

Hapa chini ni orodha ya matawi 70 ya imani kama yalivyokusanywa kutoka kwa wanazuoni wa kiislamu wenye kuaminika:

A- Matawi ya Imani ya MOYO (Itikadi) – (30)

1. Kumuamini Allah (Tawhid)
2. Kuamini Malaika
3. Kuamini Vitabu vya Allah
4. Kuamini Mitume
5. Kuamini Siku ya Mwisho
6. Kuamini Qadar (kheri na shari)
7. Kumpenda Allah
8. Kumuogopa Allah
9. Kumtumainia Allah
10. Kurejea kwa Allah (Tawbah)
11. Ikhlasi (kumtakasia Allah ibada)
12. Kuridhika na Qadar
13. Shukrani kwa Allah
14. Subira

15. Unyenyekevu

16. Kupenda kwa ajili ya Allah

17. Kuchukia kwa ajili ya Allah

18. Kuwa na Imani ya kweli (Yaqiin)

19. Kuogopa adhabu ya Allah

20. Kutarajia rehema ya Allah

21. Kuepuka kiburi

22. Kuepuka unafiki

23. Kuepuka chuki

24. Kuepuka husda (wivu mbaya)

25. Kuepuka ghadhabu isiyofaa

26. Uaminifu wa moyo

27. Haya

28. Kumuomba msaada Allah pekee

29. Upole wa moyo

30. Kuwa na nia njema

B - Matawi ya Imani ya ULIMI (Kauli) – (8)

31. Shahada ya Tauhid (Laa ilaaha illa Allah)

32. Shahada ya Mtume (Muhammad RasuluLlah)

33. Kusoma Qur’ani

34. Kumtaja Allah (Dhikr)

35. Kuomba Dua

36. Kutamka Shahada

37. Kuamrisha mema kwa ulimi

38. Kukataza maovu kwa ulimi

C - Matawi ya Imani ya MATENDO – (32)

39. Swala

40. Zaka

41. Funga ya Ramadhan

42. Hija

43. Umra

44. Jihadi (kwa sharti zake)

45. Kusaidia wanyonge

46. Ukarimu kwa wageni

47. Kuwa mwema kwa wazazi

48. Kuunganisha jamaa

49. Kusema kweli

50. Kutimiza ahadi

51. Uaminifu

52. Heshima kwa majirani

53. Kuzuia dhulma

54. Kusaidia wanaodhulumiwa

55. Kuhukumu kwa haki

56. Kusamehe

57. Kunyenyekea kwa Allah

58. Kudumisha usafi (twahara)

59. Kuvaa vizuri kwa halali

60. Kula halali

61. Kujisitiri

62. Kujiepusha na haramu

63. Kufanya kazi halali

64. Kuheshimu mikataba

65. Kumuiga Mtume

66. Kusimamisha Sharia kwa usahihi

67. Kuepuka uzushi (Bid’ah)

68. Kusaidia kazi za kheri

69. Kutoa Salamu

70. ✅ Kuondoa udhia njiani (hili ndilo la chini kabisa kama ilivyotajwa kwenye hadithi)

Hitimisho la wanazuoni

Imani inaongezeka kwa matendo mema

Imani inapungua kwa madhambi

Imani sio kauli tu, bali ni: Itikadi ya moyo + Kauli ya ulimi + Matendo ya mwili.

Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema:

"Haya ni katika Imani” [Hadithi Sahihi].

Katika hadithi nyengine “Haya haileti isipokuwa

kheri”

Mtume Swallallahu Alaihi Wasallam Amesema:
"Hatoamini (haikamiliki au haisihi imani ya mmoja wenu mpaka matamanio yake yafuate yale niliyokuja nayo" [Hadithi Sahihi].

UTAMU WA IMANI

Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema:

"Mambo matatu mwenye kuwa nayo atapata kwa mambo hayo utamu wa imani : Awe Allah (Subhanahu Wataala) na Mtume wake (Swallallahu Alaihi Wasallam) wanapendeza zaidi kwake kuliko wengineo, na ampende mtu awe hampendi isipokuwa kwa ajili ya Allah (Subhanahu Wataala) na achukie kurudi katika ukafiri kama anavyochukia kutupwa katika moto" [Hadithi Sahihi].

Wamesema Wanachuoni ‘‘Utamu wa Imani ni kupata ladha na hamu katika kumtii Allah (Subhanahu Wataala)’’yaani ni hali ya ndani ya moyo wa Muumini ya kuhisi furaha, utulivu na kujisikia amani na raha pale anapomtaja Allah (Subhanahu Wataala) na kutekeleza ibada mbali mbali.

Amesema Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam):
‘‘Ameonja utamu wa Imani Mwenye kuridhia kuwa Allah ndio Mola wake, Uislamu kuwa ndio dini yake na Muhammad kuwa ndio Mtume wake” (Sahihi).

Kuna Ishara gani au hali zipi zinamtambulisha Muislamu kuwa anapata utamu wa Imani?

Ishara za mtu mwenye kupata ladha au utamu wa Imani ni pamoja na kufurahia kumtii Allah (Subhanahu Wataala), kuepukana na maasi, kupata huzuni pale anapomkosea Allah bila kukusudia, kutulia na kujisikia raha na amani katika dhikri na ibada.

Utamu wa Imani ni kilele cha mafanikio ya muumini, yaani ni dalili kuwa moyo wa muumini umefikia kiwango cha juu cha uhusiano na Allah (Subhanahu Wataala) na hata katika shida hupata utulivu na matumaini kwa kuwa yuko karibu mno na Allah (Subhanahu Wataala).

Utamu wa Imani huituliza nafsi na kuondoa huzuni zisizokuwa na msingi za mambo ya kidunia.

Utamu wa Imani huongeza msimamo katika dini (Istiqama) na humfanya Muumini kutoyumbishwa na vishawishi vyote vya kidunia kama vile wanawake, mali, watoto, cheo, umaarufu n.k.

Utamu wa Imani humfanya Muumini awe na furaha ya kweli ambayo ni tofauti kabisa na furaha anayoipata katika jambo lolote katika mambo ya kidunia.

Jee wewe ndugu yangu muislamu, umeshawahi kuonja utamu wa imani ? unapata utulivu unapoingia katika swala ? Moyo wako hutulia Akitajwa Allah ? Jee unafurahia ukifanya wema hata usipoonekana na mtu

yeyote na unachukia unapofanya kosa bila kukusudia ? Hivi vyote ni viashiria vya Utamu wa Imani.

Utamu wa Imani kila muislamu anaweza kuifikia kupitia juhudi ya kweli na endelevu ya kumtambua, kumpenda na kumtii Allah (Subhanahu Wataala).

Utamu wa Imani hauji ghafla wala kwa kutamani bali hutengenezwa hatua kwa hatua kwa nia, juhudi na msimamo mzuri wenye kendelea katika dini.

Tunamuomba Allah (Subhanahu Wataala) Atupe ladha na utamu wa kumtii na Asituondoshe duniani mpaka Awe Ameturidhia Aamiin.

Hadithi Sahihi za Mambo ya Imani zinaendelea….

1- Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema :

"Hatoamini mmoja wenu mpaka ampendelee ndugu yake muislamu kile anachoipendelea nafsi yake" [Hadithi Sahihi].

2- Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema :

“Naapa kwa Allah, Hakuamini (mara tatu), Maswahaba Wakasema : Nani Ewe Mjumbe wa Allah ? Akasema Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam): Yule ambae hakupata amani (hakusalimika) jirani yake kutokana na shari zake” [Hadithi Sahihi].

3- Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema :

"Hatoamini mmoja wenu mpaka Mimi niwe napendeza (Ananipenda) zaidi kuliko mzazi wake, mtoto wake na watu wote" [Hadithi Sahihi].

4- Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema :

"Mwenye kumuamini Allah (Subhanahu Wataala) na siku ya mwisho basi amkirimu (amfanyie wema) jirani yake, Mwenye kumuamini Allah (Subhanahu Wataala) na siku ya mwisho basi amkirimu mgeni wake na Mwenye kumuamini Allah (Subhanahu Wataala) na siku ya mwisho basi aseme (azungumze) kheri au (kama hana) anyamaze kimya (aepukane na shari za ulimi wake)" [Hadithi Sahihi].

5- Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema:

"Mwenye kuuona uovu basi auzuie kwa mkono wake (kama ana mamlaka), kama hawezi basi auzuie kwa ulimi wake (aseme) na kama hawezi basi kwa moyo wake (achukie) na huko kuchukia ni udhaifu mkubwa wa imani (ya mja)" [Hadithi Sahihi].

6- Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema :

"Hamtoingia Peponi mpaka muamini (muwe na imani sahihi) na hamtoamini mpaka mupendane ! Je nikufahamisheni jambo ambalo mukilifanya mutapendana ? Toleaneni salamu baina yenu" [Hadithi Sahihi].

7- Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema :

"Mambo matatu ni katika imani : Kutoa swadaka, kutoa salamu na kuichunga nafsi yako" [Hadithi Sahihi].

8- Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema :

"Mwenye kupenda kwa ajili ya Allah (Subhanahu Wataala), akachukia kwa ajili ya Allah (Subhanahu Wataala), akatoa kwa ajili ya Allah (Subhanahu Wataala) na akazuia kwa ajili ya Allah (Subhanahu Wataala) basi hakika imekamilika imani yake" [Hadithi Sahihi].

9- Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema :

“Ajabu ilioje kwa mambo ya Muumini, Hakika mambo yake yote ni kheri tupu, na hali hiyo haiwi kwa yeyote isipokuwa Muumini tu, ikimpata kheri hushukuru na inakuwa kheri kwake na likimpata dhara (jambo lolote lenye kuchukiza) husubiri na inakuwa kheri kwake !” [Hadithi Sahihi].

10- Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema :

"Mkamilifu wa imani katika waumini ni yule mwenye tabia nzuri zaidi" [Hadithi Sahihi].

11- Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema :

"Muislamu wa kweli ni yule ambae waislamu wenzake wamesalimika kutokana na (shari ya) ulimi wake na

mkono wake, Muumini wa kweli ni yule ambae wamemuamini watu juu ya damu zao na mali zao na mwenye kuhama ni yule mwenye kuyahama aliyokataza Allah (Subhanahu Wataala)" [Hadithi Sahihi].

12-Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema :

"Kumtukana muislamu ni ufasiki (uasi) na kupigana nae ni ukafiri" [Hadithi Sahihi].

13-Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema :

"Anapozini mja, imani inamtoka (moyoni) na inakaa juu ya kichwa chake kama kivuli, na anapoacha inamrejea" [Hadithi Sahihi].

14-Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema : "Hazini mwenye kuzini wakati ule anazini akiwa ni muumini (Mwenye Imani ya kweli) na hanywi ulevi mwenye kunywa wakati ule anakunywa akiwa ni muumini na haibi mwenye kuiba wakati ule anaiba akiwa ni muumini" [Hadithi Sahihi].

FAIDA ZA IMANI

1- Allah (Subhanahu Wataala) Amesema "Mwenye kufanya matendo mema akiwa mwanamme au mwanamke hali ya kuwa ni muumini [Mwenye Imani ya kweli iliyotulia moyoni], basi tutamfanya aishi

maisha mazuri na kwa hakika tutawalipa huko Akhera malipo yao kwa uzuri zaidi ya yale mazuri waliokuwa wakiyafanya (duniani)” Qur’ani [16:97].

2-Allah (Subhanahu Wataala) Amesema “Hakika wale walioamini (wenye Imani ya kweli iliyotulia moyoni) na wakafanya matendo mema (kwa viungo vyao baada Imani kutulia moyoni) makaazi (mafikio) yao yatakuwa katika hizo Pepo za Firdaws, watakaa humo milele hawatotaka kuondoka” Qur’ani [18:107-108].

3-Allah (Subhanahu Wataala) Amesema “Hakika wale walioamini (wenye Imani ya kweli iliyotulia moyoni na wakafanya matendo mema (kwa viungo vyao baada Imani kutulia moyoni) watakuwa na Pepo zenye kudumu, watakaa humo milele. Ahadi ya Allah (Subhanahu Wataala) ni kweli (ni muhali kwenda kinyume na ahadi yake) na Yeye Allah (Subhanahu Wataala) ni Mshindi (katika amri zake) na Mwenye hekima (katika uendeshaji na usimamiaji wa mambo yake)” Qur’ani [31:8-9].

4-Allah (Subhanahu Wataala) Amesema “Naapa kwa Zama au wakati unaomalizika kwa haraka sana, Hakika Mwanadamu (Yeyote) yumo katika khasara (ya kuangamia), isipokuwa wale walioamini [Wenye Imani ya kweli iliyotulia moyoni] na wakafanya matendo mema [Kwa viungo vyao vyengine baada Imani kutulia

katika moyo] na wakausiana (kuhimizana) katika kushikamana na Haki [Kheri zote kubwa na ndogo] na wakausiana (kuhimizana) katika kushikamana na Subra [Kusubiri katika kumtii Allah (Subhanahu Wataala) kwa kutekeleza maamrisho, kujizuia na makatazo na kuvumilia katika misiba, maradhi, mabalaa na maudhi ya watu. Hao wenye sifa hizo nne hawamo kabisa katika jumla ya watu waliopata khasara ya kuangamia bali wamesalimika na wameokoka katika maisha yao ya mpito ya duniani na maisha ya milele ya akhera]” Qur’ani [103:1-3].

Ni mara ngapi Allah (Subhanahu Wataala) Amewataja kwa wema na mafanikio makubwa katika Qur’ani Wale waliomuamini (wenye Imani ya kweli) na wakafanya matendo mema? bila shaka ni mara nyingi sana, yote ni kuonyesha umuhimu mkubwa mno usio na kifani kwa mja kuwa na Imani Sahihi Moyoni iliyothibitishwa na matendo mema katika maisha haya ya mpito ya duniani.

Muislamu Yeyote mwenye kujitambua anafahamu na anauhisi umuhimu wa Imani na Matendo mema katika maisha yake, bali ukweli ulivyo ni kuwa mafanikio na kheri zote za maisha ya mpito ya duniani na maisha ya milele ya akhera yatapatikana kwa Muislamu kuwa na imani sahihi iliyothibitishwa na matendo mema na hilo ndio jambo kubwa la mwanzo analotakiwa Muislamu

Yeyote kulipa kipao mbele katika maisha yake kwa kuwa nalo kama hana kulitafuta na kulihifadhi kwa mujibu wa uwezo wake aliopewa na Allah (Subhanahu Wataala) kwa sababu ndilo pekee litakalomfanya aishi maisha mazuri duniani, aepukane na maasi, shari, aweze kufanya matendo mema kwa wepesi na apate malipo mema ya Akhera na neema zake zenye kudumu milele.

Kwa masikitiko makubwa ni kuwa zama hizi waislamu tulio wengi hatuoni umuhimu wowote wa kutafuta njia za kutafuta, kutengeneza, kulinda na kuimarisha imani zetu! na hilo linaonekana wazi katika matendo na mahusiano yetu baina yetu na Mola wetu Aliyetuumba, kila mmoja wetu ameghafilika na kushuhgulishwa katika kutafuta wingi wa mali, jaha na kupoteza muda wake wote katika mambo ya upuuzi na batili, mambo ambayo ukiyaangalia hayana faida yoyote katika maisha ya mpito ya duniani na maisha ya milele ya Akhera.

“Watu wamelala (wameghafilika) na pale wanapokufa ndio huzinduka (wakaona umuhimu mkubwa mno wa Imani na Matendo mema)’’ na hapo ndio hujuta (kwa kuupoteza muda wao wote katika mambo ya upuuzi na batili) na wanapojuta hayo majuto hayawasaidii kwa chochote [Aliy bin Abi Talib, Allah Amridhie].

Allah Subhanahu Wataala Amesema : ‘Allah (Subhanahu Wataala) Amewaahidi wale walioamini (wenye imani) wanaume na wanawake mabustani ya Pepo ambayo chini yake inapita mito, watakaa humo milele na majumba yaliyojengwa vizuri yenye utulivu katika mabustani yenye kudumu. Na radhi za Allah (Subhanahu Wataala) ndio jambo kubwa zaidi. Huko ndiko kufuzu (kufaulu) kukubwa" Qur’ani [9:72]. Allah Subhanahu Wataala Amesema "Kwa hakika (yakini) wale walioamini (wenye imani) na kufanya vitendo vizuri, makazi yao yatakuwa hizo Pepo za Firdaws; watakaa humo milele, hawatotaka kuondoka" Qur’ani [18:107-108] Aya kama hizi zimo nyingi sana katika Qur'ani hatuwezi kuziweka zote hapa.

Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema :

“Hakika Watu wa Peponi wataonyeshana majumba ya watu wa peponi kama mnavyoonyeshana nyota za mashariki (ya anga ya mbali) au magharibi kutoka ardhini (duniani), kwa kule kutofautiana kwa yale waliyonayo. Wakasema Maswahaba: Ewe Mjumbe wa Allah hayo ni makaazi ya Mitume ambayo hawawezi kuyafikia watu wengine? Akasema Mtume (Swallahu Alaihi Wasallam): Hapana! Naapa kwa Yule Ambae nafsi yangu ipo mikononi Mwake, hayo ni makaazi ya Watu Waliomuamini Allah (Subhanahu Wataala) na

Wakawaamini Mitume wa Allah (Subhanahu Wataala)” [Sahihi Bukhari Nambari 3256 na Muslim 2831].

UMUHIMU WA IMANI KATIKA JAMII

Ustawi na mafanikio ya duniani na akhera ya jamii yoyote yanategemea imani kwa maana ikikosekana imani hakuna ustawi na mafanikio kwa waislamu duniani na akhera ndio maana Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Alitumia zaidi ya miaka 10 katika mji wa Makka baada kupewa utume kuwajenga wafuasi (maswahaba) wake IMANI mpaka wakamtambua Allah (Subhanahu Wataala) na ndio maana kwa sababu ya nguvu ya IMANI na UMOJA (UDUGU) wao waliufikisha uislamu walipoufikisha hata baada ya kuondoka Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) hatimaye mimi na wewe tumeipata neema ya Uislamu.
Allah (Subhanahu Wataala) Amesema :
"Allah (Subhanahu Wataala) Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na wakafanya matendo mema kwamba atawarithisha ardhi ya washirikina na atawafanya ni wasimamizi wa hiyo ardhi, kama alivyofanya kwa waliokuja kabla yao kati ya wale waliomuamini Allah na Mitume Wake, na Aifanye dini yao ambayo Ameridhika nayo na Akawachagulia, nayo ni Uislamu ni dini yenye ushindi na uthabiti, na Azigeuze hali zao kwa kuwaondolea khofu na kuwaletea amani, wamuabudu Allah bila kumshirikisha

na kitu chochote. Na Mwenye kukanusha [baada ya hilo la kupewa usimamizi, amani, uthabiti na utawala kamili, na akakanusha neema za Allah, basi hao ndio waliotoka nje ya utiifu kwa Allah" Qur'ani [24:55].

"...Hakika Allah Hageuzi neema aliyowaneemesha watu mpaka wao wenyewe wageuze walioamrishwa na Mola wao na wakamuasi. Na Allah Akiwatakia watu mtihani (majaribio) basi hakuna namna ya kuyakimbia, na hawana wao asiyekuwa Allah msimamizi yeyote wa kuyasimamia mambo yao, akawaletea wanayopenda na akawakinga na wanayochukia" Qur’ani [13:11].

IMANI ikitulia katika moyo, maasi yote ya moyo kama vile unafiq, shaka, kibri, husda, choyo, chuki, kujiona, kujionyesha, khasira, ukatili, ubakhili, uvivu, pupa, tamaa, kupenda mno mali, kupenda mno dunia na maaswi mengine yanakimbia mbali na yale matendo mazuri ya moyo kama vile Taqwa (uchamungu), ikhlasw (kumkusudia Allah katika ibada), khushui (unyenyekevu), upole, haya, kusamehe, kukinai, tawakkul (kumtegemea Allah) na kadhalika ndio yanatawala katika moyo wa muislamu.

Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema :

"...Tambueni hakika katika mwili kuna kipande cha nyama kikitengenea hutengenea mwili mzima na kikiharibika huharibika mwili mzima, tambueni kuwa huo ni MOYO..." (Hadithi Sahihi).

Kwa maana ya kawaida (kihisia) ni kweli kuwa moyo ndio kiungo muhimu sana katika mwili wa mwanadamu na kwa maana iliyokusudiwa ni kwamba MOYO ukitengenea kwa kujaa IMANI na ELIMU basi mwili wote nao hutengenea kwa kutenda yale yaliyoamrishwa na kuacha yale yaliyokatazwa na Allah (Subhanahu Wataala) na Moyo ukiharibika kwa kukosa imani (na kutawaliwa na maasi ya moyo) mwili mzima nao huharibika kwa kuingia katika maasi mbali mbali ya viungo ambapo viungo viwili hatari zaidi kwa kauli ya Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) ni ulimi ukifuatiwa na utupu hali ya kuwa njia ya kuuhifadhi ulimi ni mtu kunyamaza kutokana na mengi anayosema na njia ya kuuhifadhi utupu ni kuhifadhi macho yasiangalie yaliyoharamishwa.
Tunamuomba Allah Azijaze nyoyo zetu nuru ya IMANI na aziepushe mbali na maaswi. Aamiin.

HALI ZA MOYO WA MWANADAMU

Hali za moyo wa mwanadamu ni tatu, hakuna ya nne kwa hivyo itafute hali ya moyo wako hapa:

1-HALI YA MOYO ULIOSALIMIKA:

Hali ya Moyo ambao hawezi kuokoka na adhabu siku ya kiyama mja yeyote isipokuwa atakayemuendea Allah (Subhanahu Wataala) na moyo wenye hali hii.
Hali ya Moyo huu Ameitaja Allah Aliposema:

"Siku (ya kiyama) ambayo mtu haitomfaa mali yake wala watoto, isipokuwa yule atakaemjia Allah akiwa na moyo uliosalimika" Qur’ani [26:88-89].

Kwa ufupi moyo huu ni ule uliosalimika na ukafiri, shirki, shaka, unafiq na kila matamanio yanayokwenda kinyume na amri za Allah - Ukipenda unapenda kwa ajili ya Allah, ukichukia unachukia kwa ajili ya Allah, ukitoa unatoa kwa ajili ya Allah, ukizuia unazuia kwa ajili ya Allah, ukizumgumza, ukinyamaza, ukilala, ukiamka, ukifanya kazi, ukipumzika, ukifikiri na mengineyo yote unafanya kwa ajili ya Allah.

Waumini wa kweli waliotajwa katika Qur'ani (8 :2-4), (23 :1-11), (49 :15) na kadhalika ndio wenye moyo wa aina hii. Tunamuomba Allah (Subhanahu Wataala) Atupe moyo wa aina hii Aamin.

2-MOYO ULIOKUFA:

Moyo huu ni kinyume cha moyo uliosalimika:

Yaani ni moyo ambao haumtambui (haumuamini) wala haumuabudu Mola wake bali hufanya kila kitu kwa kufuata matamanio yake. Makafiri waliotajwa katika Qur'ani (2:6-7) na nyenginezo nyingi ndio wenye moyo wa aina hii.

Tunamuomba Allah (Subhanahu Wataala) Atukinge na moyo wa aina hii Aamiin.

3-MOYO WENYE MARADHI:
Ni moyo wenye uhai (imani dhaifu sana) na unasumbuliwa na baadhi ya maradhi (maasi) mbali mbali ya moyo: shaka, unafiq, kibri, husda, choyo, chuki, kujiona, ubakhili, kujionyesha, ufisadi, ubinafsi, tamaa, khasira, ukatili, uvivu, kupenda mno mali, kupenda mno dunia n.k. Imani ikitawala (ikishinda) ndio unapata uhai na kuelekea kwenye moyo uliosalimika na maradhi (maasi) yakitawala (yakishinda) ndio unaelekea kwenye moyo uliokufa.
Tiba ya moyo huu ili usalimike ni Qur'ani kwa sababu ndio inayotibu maradhi yote ya moyoni.
Allah Amesema: "Enyi watu yamewajia mawaidha (Qur'ani) kutoka kwa Mola wenu na tiba (dawa) ya yale yaliyomo vifuani (nyoyoni katika shirki, unafiq, shaka na maradhi mengine), na mwongozo na rehema kwa waumini (wenye imani)" Qur’ani [10:57].

Pia Allah Amesema: ‘‘Na tumeteremsha katika Qur’an yale ambayo ni ponyo (tiba) na rehema kwa waumini na wala haitowazidishia (hii Qur’an) waliodhulumu isipokuwa khasara’’ Qur’an [17:82].
Wanachuoni Wamesema:
Tiba ya moyo ni kufanya mambo matano (5):
1-Kusoma Qur'ani kwa kuizingatia maana yake.
2-Tumbo kuwa wazi kwa kukithirisha kufunga.
3-Kuswali usiku watu wakiwa wamelala.

4-Kunyenyekea wakati wa kula daku kwa kuomba dua, kumtaja Allah, kuomba msamaha (Istighfar) n.k.
5-Kukaa na watu wema.

Amesema Imam Tirmidhiy (Allah Amrehemu): "Uhai wa moyo ni imani na kufa kwake ni ukafiri, uzima wake ni kumtii Allah na maradhi yake ni kumuasi Allah, kuamka kwake ni kumkumbuka Allah na kulala kwake ni kughafilika kumkumbuka Allah". Tunamuomba Allah Atupe imani katika nyoyo zetu na Atufanye tuchukie ukafiri na kumuasi-Aamiin.

UDHAIFU WA IMANI

DALILI, SABABU NA TIBA YAKE

Ni jambo lililo wazi kuwa tatizo la udhaifu wa imani ni tatizo lililoenea kwa waislamu tulio wengi kama sio wote, kila mmoja wetu bila shaka anauhisi ugumu wa moyo wake kwa kutoathiriwa na mawaidha, Qur'ani, mauti, kuingia katika maasi kwa wepesi na kuhisi ugumu na uzito katika kuziendea ibada za faradhi kama vile swala tano khasa swala ya alfajiri, kutoa kwa ajili ya Allah (Subhanahu Wataala) n.k, hayo yote yanasababishwa na udhaifu mkubwa wa imani zetu.

Hizi hapa ni dalili, sababu na tiba za udhaifu wa imani :

DALILI ZA UDHAIFU WA IMANI

Hakika udhaifu wa imani una dalili nyingi katika hizo ni hizi zifuatazo kwa ufupi:

1-Kuingia kwa wepesi katika maasi na kufanya mambo yaliyoharamishwa.
2-Kuhisi ugumu wa Moyo mpaka anahisi mtu moyo wake umekuwa kama jiwe! hauathiriwi na mawaidha wala Qur'ani wala mauti n.k.
3-Kuhisi uzito na uvivu katika kuziendea ibada mbali mbali.
4-Kughafilika kumkumbuka na kumtaja Allah.
5-Kudharau na kutojali mambo yanayowahusu waislamu kama kwamba hayakuhusu.
6-Kufadhaika, kupata khofu na kutostahamili wakati wa misiba.
7-Kutawaliwa na maasi ya moyo: kibri, husda, kujionyesha, chuki, kujiona, ubakhili, uvivu, kupenda mno dunia, kupenda mno mali n.k.

SABABU ZA UDHAIFU WA IMANI

Udhaifu wa imani una sababu nyingi miongoni mwa hizo ni:
1-Kuwa mbali na mazingira ya kiimani kwa mfano mtu ambae amekuwa mbali na ndugu zake waumini au mlezi wake wa kiimani anakosa muendelezo na ustawi wa imani yake.
2-Kuacha kujishughulisha na kutafuta elimu yenye manufaa yaani elimu ya kumtambua Mola wako, Dini yako na Mtume wako ambayo chimbuko lake ni Qur'ani na Hadithi sahihi.
3-Kuingia katika sehemu za maasi mfano katika maholi ya starehe za miziki, ulevi, zinaa n.k.
4-Kushughulikia zaidi dunia ya muda mfupi mpaka

ukawa huna wakati wa kushughulikia dini na akhera yako yenye kudumu mfano kupoteza muda wote katika kushughulikia mali yako, mke wako na watoto wako. Maana yake ni kuwa vitu hivi vikakushughulisha ukaacha kumtii Mola wako.
5-Matarajio na mipango mingi ya kidunia ambayo mara nyingi inakusahaulisha kuyakumbuka mauti na mambo ya akhera.
6-Marafiki waovu kwa sababu mtu mara nyingi humfuata rafiki yake akamshughulisha na akamueka mbali na Mola wake.
7-Kukithirisha kula (na kunywa), kulala na kuchanganyika ovyo na watu.
Imesemwa kuwa "Mwenye kula sana atakunywa sana, atalala sana na hatimae atakosa ujira mkubwa wa matendo mema" na maneno mengi yasio na faida yanaufanya moyo uwe mgumu, kuchanganyika sana na watu kunamueka mtu mbali na Mola wake na kucheka sana kunaufisha moyo.

TIBA YA UDHAIFU WA IMANI

1-Kuizingatia Qur'ani.

Hakuna shaka yoyote kuwa Qur'ani ni tiba kubwa ya maradhi yote ya moyo, na njia ya kujitibu kwa kutumia Qur'ani ni kuitafakari na kuizingatia kwa makini wakati wa kuisoma na kuisikiliza.

2-Kuuhisi ukubwa na utukufu wa Allah (Subhanahu Wataala) kwa kujua na kuzingatia majina na sifa za Allah (Subhanahu wataala) na kufikiria ukubwa na utukufu wa Allah (Subhanahu Wataala) katika uumbaji

wa viumbe mfano dunia na vilivyomo vya nchi kavu na baharini, jua, nyota, sayari, mwezi, usiku na mchana na mengineyo mengi yanayoonyesha ukubwa na utukufu wa Allah (Subhanahu Wataala) ambayo yanaonekana kwa macho ambayo pia yameelezwa katika Qur'ani [Rejea: Dalili za kuwepo Allah (Subhanahu Wataala)].

3-Kujishughulisha katika kutafuta elimu yenye manufaa ambayo ni elimu itakayokufanya umuogope Allah na kuzidisha imani yako nayo ni elimu inayotokana na Qur'ani na hadithi sahihi za Mtume Swallallahu Alaihi Wasallam.

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema:

"...Hakika wanaomuogopa Allah katika waja wake ni wale wanaomtambua (Wanazuoni)..." Qur'ani [28:28]

Vipi watakuwa sawa katika imani wale wanaojua baada ya kusoma nini kitatokea baada mauti katika fitna za kaburi na hali za siku nzito ya kiama, na neema za pepo na adhabu za moto na wale wasiojua ?

4-Kujilazimisha kumkumbuka na kumtaja sana Allah (Subhanahu Wataala), nako kuna athari ya ajabu katika kuzidisha imani ya mja kwa sababu mtu mwenye kupenda jambo hukithirisha kulikumbuka na kulitaja kwa hivyo kukithirisha kumkumbuka na kumtaja Allah (Subhanahu Wataala) ni ishara ya kuwepo Imani katika Moyo, kila utajo wa Allah (Subhanahu Wataala) ukiengezeka na Imani nayo inaongezeka kwa kiasi kile kile cha utajo wa Allah (Subhanahu Wataala).

5-Kukithirisha kufanya matendo mema kwa kuyakimbilia na kuyadumisha japo kuwa ni machache.

Kuutumia muda mwingi katika mambo mbali mbali ya kheri mfano kuwafanyia ihsani wazazi, kuamiliana vizuri na mke, watoto, majirani, kuwatembelea wagonjwa, kuzuru makaburi kwa wanaume, kuunga udugu, kuwalisha masikini, mayatima na mambo mengine mengi ya kheri ya kuimarisha imani na wakati.

6-Kuogopa mwisho mbaya ambao sababu yake kubwa ni kudhoofika kwa imani na kuzama katika maasi mbali mbali.

7-Kufanya wingi wa kuyakumbuka mauti:

Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema: "Fanyeni wingi wa kukikumbuka kitu chenye kukata ladha (yaani mauti)" [Hadithi Sahihi].

Mtu akikumbuka kuwa kuna siku na mimi nitakufa tu kama wanavyokufa wenzangu na nitauonja uchungu wa mauti kama walivyoonja wenzangu! basi kunamfanya mtu aogope kumuasi Allah (Subhanahu Wataala) na kunaulainisha moyo wake na katika mambo yanayomkumbusha mtu mauti ni kuhudhuria katika mazishi na kutembelea makaburi.

Mtu mwenye kuyakumbuka sana mauti humjia mambo matatu:

1-Huharakisha kutubia na kuleta istighfar kabla mauti hayajamvaa.

2-Kukinai na kile alichomruzuku Allah na kupunguza pupa ya mali na mipango mingi ya mambo ya kidunia.

3-Uchangamfu katika kumtii Allah na kuziendea ibada mbali mbali.

Na kinyume chake ni kweli mtu yeyote yule mwenye kuyasahau mauti mambo matatu (3) na yeye vile vile

yatamvaa tu:
1-Kuichelewesha toba mpaka yanamvaa mauti bila kutubia.
2-Kufanya uvivu katika ibada na kumtii Allah.
3-Kutokinai na kile Allah Alichomruzuku na kufanya pupa ya mali na mipango mingi ya mambo ya kidunia kama kwamba ataishi milele ilhali wakati wowote anaweza kuondoka akiwa hajatekeleza lolote katika mambo mengi aliyopanga.
Ndugu Yangu Muislamu, safari hii (mauti) ni safari ya hatari sana! ni safari ya ghafla ambayo haina wakati maalum bali ni wakati wowote, haina umri maalum bali ni umri wowote na haina pahala maalum bali ni pahala popote na wala haina hali maalum ni hali yoyote ya ugonjwa na uzima umejiandaa au hukujiandaa unakwenda tu! Tunamuomba Allah (Subhanahu Wataala) Atupe mwisho mwema Aamiin.

ATHARI ZA MAASI (MADHAMBI)

Maasi au Madhambi tunayofanya usiku na mchana, kwa siri na dhahiri na kwa kujua na kutojua yana athari mbaya mno kwa mtu katika moyo wake, katika dini yake, katika riziki yake, katika nafsi yake (mtu pekee) na katika jamii nzima kwa ujumla kama ambavyo kumtii Allah (Subhanahu Wataala) na matendo mema yana athari njema mno na faida nyingi katika nyanja zote hizo zilizotajwa.
KWA MOYO WAKE:
Maasi yanarithisha upweke, kiza, udhalilifu, maradhi

mbali mbali katika moyo [Shaka, Unafiq, Kibri, Husda, kujiona n.k] na yanamueka mbali mja na Allah.

KWA DINI YAKE:

Maasi yanamkosesha mtu kumtii Allah, kukubaliwa matendo yake na kunufaika na dua ya Mtume, Malaika na Waumini.

KWA RIZKI YAKE:

Maasi kwa kweli yanaondosha baraka katika rizki na yanaondosha neema na baraka ya mali. Unaweza ukawa na kipato kikubwa lakini ukajiona masikini na unaweza ukawa na kipato kidogo lakini ukajiona tajiri.

KWA MTU MMOJA MMOJA:

Maasi yanaondosha baraka ya umri, yanarithisha maisha magumu na mambo kuwa magumu.

KWA JAMII:

Maasi yanaondosha neema ya amani, yanavutia umasikini, majanga, mabalaa, kusalitishiwa maadui na viongozi wabaya wasio na huruma kwa raia wao n.k.

MAASI YA MOYO NA VIUNGO VYENGINE

Ni muhimu sana kuelewa kuwa sisi viumbe tunamuasi Muumba ambae ni Allah (Subhanahu Wataala) kwa kutumia viungo mbali mbali ambavyo ni neema na amana kwetu!

Kuzitumia neema hizi katika kumuasi Yule Aliyetupa ni Ukafiri mbaya mno na kuifanyia khiyana amana aliyotuazima ni Uasi mkubwa sana!

Tumefahamu bila shaka kwa ufupi athari mbaya mno za Maasi, hapa utapata kufahamu baadhi ya maasi yanayofanywa na viungo mbali mbali katika mwili wa mwanadamu kama vile moyo, ulimi na viungo vyengine ili tufanye bidii ya kujiepusha nayo kwa msaada na rehema za Allah Subhanahu Wataala.

MAASI YA MOYO

Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema katika hadithi sahihi kuwa:
"…Tambueni kuwa katika mwili kuna kipande cha nyama, kikitengenea hutengenea mwili mzima na kikiharibika basi mwili mzima nao huharibika, tambueni kuwa huo ni Moyo…" [Hadithi Sahihi].

Maasi ya Moyo yaliyoenea katika jamii zetu ni haya yafuatayo:

1- KIBRI

Ndio dhambi ya kwanza kutendeka huko mbinguni! Nayo ni pale Iblis alipokataa kumsujudia Baba yetu Adam kwa kibri cha kujiona Yeye ni bora na anastahiki zaidi kusujudiwa kuliko Nabii Adam na maana yake kwa ufupi ni Kujikweza na kujiona wewe ndio wewe na wengine wote hawana maana.
Mtume Amesema katika hadithi sahihi kuwa:
"Hatoingia peponi mwenye chembe ya kibri katika moyo wake" Vile vile Amesema:
"Kibri ni kuikataa Haki na kuwadharau watu"

Mtume Pia Amesema kuwa "Mwenye kuanza kumtolea salamu (ndugu yake Muislamu) kwa hakika Ametakasika(Ameepukana) na kibri!"
Tunamuomba Allah (Subhanahu Wataala) Atukinge na gonjwa hili baya mno la moyo Aamiin.

2- HUSDA

Ndio dhambi ya kwanza iliyoanzishwa ardhini pale Kaabil alipomuhusudu ndugu yake Haabil ikampelekea kuanzisha kitendo kibaya cha kuua!
Maana yake kwa ufupi ni kuchukia neema ya mwenzako na kutaka imuondekee.
Kwa hivyo ukamfanyia uadui ili aikose hata kama na wewe utaikosa! Ubaya ulioje huu!

Mkasa:

Katika ubaya wa Husda, Watu wanasimulia kuwa Hasidi aliambiwa achague chochote anachotaka lakini kwa sharti ya kuwa mwenzake atapewa mara mbili ya alichochagua!
Hakuwaza kuchagua neema yeyote bali kinyume chake alichagua kutolewa jicho lake moja ili kusudi mwenzake atolewe yote mawili!
Imesemwa vile vile kuwa ukimuona mtu anakwambia “Maa-Shaa-Allah” kwa uso wenye furaha baada ya kumtajia neema yako ambayo Yeye hanayo basi hiyo ni ishara kuwa amefurahia neema yako kwa hivyo ametakasika (ameepukana) na hasad na ukimuona

kabadilika kwa hasira basi atakuwa amechukizwa na neema yako kwa hivyo ni Hasidi!
Tunamuomba Allah (Subhanahu Wataala) Atukinge na gonjwa hili baya mno la moyo! Aamiin.

3- CHUKI

Ni kumchukia ndugu yako bila sababu ya msingi. Hii baadae hupelekea mpaka mtu anakuwa na hasad kwa ndugu yake.

4- KUJIONYESHA

Ni shirki ndogo, maana yake ni kutafuta cheo, utukufu, heshima katika nyoyo za watu!
Ndio utawaona watu wanafanya mpaka matendo mema kwa ajili ya watu ili wayapate hayo.

5- KUJIONA

Maana yake ni kujistaajabia wewe mwenyewe na kujiona labda wewe ni mtu wa daraja la juu (High Class) na wala hustahiki kuchanganyika na watu wengine!

6- UNAFIQ

Ni ile hali ya kudhihirisha Uislamu kwa vitendo na kuficha ukafiri moyoni, Rejea...Alama za Mtu Mnafiki.

7- SHAKA

Kumfanyia Shaka Allah na Mtume wake.

8- KUPENDA MNO DUNIA

Kupenda mno dunia mpaka ukasahau kuwa dunia ni

bandia na kwamba ghafla unaweza kuiacha au kukuacha!

9- KUPENDA MNO MALI

Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema: "Kila umma una fitna yake na fitna ya umma wangu ni mali" Wengi wetu kama sio wote ugonjwa huu tunao!

10- MAASI YOTE

Ni maradhi ya moyo yaliyopea mpaka inampelekea mtu kufanya maasi mbali mbali. Hayo ni baadhi tu ya Maasi ya Moyo na mengine ni kukata tamaa na rehma ya Allah, kujiaminisha na adhabu ya Allah, choyo, khasira, ubakhili, uvivu, ukatili, khiyana, dhana mbaya n.k.

🗣 *MAASI YA ULIMI*

Uongo, ufisadi, fitna, kuamrisha uovu mfano: Piga! watu wakapiga japo kwa dhulma, Ua! watu wakaua pasi na haki!, kusengenya (kumsema mtu kwa namna ambayo atachukia iwapo atasikia hata kama ni kweli na kama si kweli itakuwa umemsingizia ambayo ndio mbaya zaidi), Ushindani katika mijadala, kuwapinga watu katika jambo la kweli, kujisifu, kulaani, mzaha, kejeli, tashtiti (inda) n.k. Asilimia kubwa ya madhambi anayofanya mja ukitoa moyo yanasababishwa na ulimi.

MAASI YA TUMBO

Kula haramu mfano kula riba, kunywa ulevi, chakula cha kuiba n.k

MAASI YA JICHO

Kuangalia wanawake wa kando, kuangalia tupu,

kuangalia kwa njia ya kudharau n.k

MAASI YA SIKIO

Kusikiliza watu wanaosengenya, wanaosingizia, miziki n.k

MAASI YA MIKONO

Kupunguza vipimo, kuiba, kupiga, kuua n.k

MAASI YA MIGUU

Kwenda kwa ajili ya kufanya ufisadi, kuua, kumdhuru muislamu n.k

MAASI YA UTUPU

Zinaa, Liwati n.k

MAASI YA VIUNGO ZAIDI YA KIMOJA

Kuwaasi wazazi, kukimbia katika vita, kukata udugu, dhulma ambayo yote ni katika madhambi makubwa! Tunamuomba Allah (Subhanahu Wataala) Atupe Uongofu na Uchamungu Atukinge na Maasi yote makubwa na madogo tunayoyajua na tusiyoyajua, ya wazi na siri, Aamiin

⚠ MADHAMBI MAKUBWA

Hii ni orodha kamili ya Madhambi Makubwa 70 kama alivyoyataja Imam Shamsuddin adh-Dhahabi katika kitabu chake mashuhuri Al-Kabā’ir:

1. Kumshirikisha Allah Subhanahu Wataala (Shirk) – Dhambi kubwa kabisa.

2. Kuuwa bila haki
3. Uchawi
4. Kuacha swala
5. Kuacha kutoa Zaka bila udhuru
6. Kuacha kufunga Ramadhan bila udhuru
7. Kuacha kwenda Hijja pamoja na kuwa na uwezo
8. Kuwakosea/Kuwaasi wazazi
9. Kukata udugu wa jamaa
10. Zina (Uzinzi)
11. Liwaat (ushoga)
12. Kula riba
13. Kula mali ya yatima
14. Kusema uongo juu ya Mtume ﷺ
15. Kukimbia vita kwa woga (kutoka mstari wa mbele)
16. Ujambazi wa barabarani (haraba)
17. Kunywa pombe na vitu vinavyolewesha
18. Kuwasema vibaya wanawake wema (Qadhf)
19. Kula kiapo cha uongo
20. Kula rushwa
21. Kula mali kwa udanganyifu wa mizani (Tatfif)
22. Kujipa mali ya umma (ghulul)
23. Kutoa ushahidi wa uongo
24. Kuvunja ahadi
25. Kula mali ya haramu hata kama si riba

26. Wizi
27. Kunyang’anya mali kwa nguvu
28. Kula njama dhidi ya mali ya watu
29. Kuwadhulumu watu katika ardhi au mali
30. Kuchelewesha kulipa deni
31. Kumsengenya mtu (Ghiba)
32. Kuchochea maneno (Namima)
33. Kusema uongo
34. Kukufuru neema (kutokushukuru neema za Allah)
35. Kujiona (ujub)
36. Kiburi na dharau
37. Hasad (husda ya kutamani mwenzako apate balaa)
38. Ujinga wa dini na kufanya mzaha na dini
39. Kumsema vibaya swahaba wa Mtume ﷺ
40. Kuwafitinisha watu
41. Kuwatukana wazazi
42. Kuwadhulumu wake/waume
43. Kuwa na uadui usio wa haki ndani ya familia
44. Kuwaingilia wanawake kinyume na maumbile
45. Kumtelekeza mke bila haki
46. Kupuuza malezi ya watoto
47. Kupitiliza adhabu kwa watoto au wake
48. Kutenganisha wanandoa kwa fitna
49. Kuoa wanawake ambao ni haramu kuwaoa

50. Kula mali ya mke bila ridhaa
51. Kuhukumu kwa hukumu isiyokuwa ya Allah
52. Kiongozi kudhulumu raia
53. Kiongozi kupewa uongozi bila sifa
54. Kuficha ushahidi wa haki
55. Kuvuruga amani ya nchi kwa fitina
56. Kupandisha bei kwa makusudi ili kuumiza watu (Ihtikaar)
57. Kuchukua kodi haramu na hongo kwa nguvu
58. Kuwazuilia watu haki zao za msingi
59. Kueneza uvumi wa uongo
60. Kuiga watu waovu (tashabbuh) kwa makusudi
61. Kuidharau Qur’ani
62. Kuivunja amana
63. Kupiga ramli / kusoma nyota (astrology)
64. Kutumia hirizi kwa imani ya shirki
65. Kutotubu madhambi makubwa
66. Kutoogesha maiti au kutozika ipasavyo
67. Kuicheka maiti au kucheka juu ya msiba
68. Kukata tamaa kabisa na rehema ya Allah (qanut)
69. Kujiaminisha (Kujiona salama mno) na adhabu za Allah Subahanahu Wataala
70. Kufanya dhambi kwa kujionyesha (mujahara)

MPANGILIO MZURI

Huu ni mpangilio wa madhambi makubwa na madhambi madogo kama yalivyoelezwa na wanazuoni wa Kiislamu wanaoaminika kama Imam adh-Dhahabi, Ibn Taymiyah, Ibn Qayyim, Imam Nawawi, na wengineo.

MADHAMBI MAKUBWA (KABAIR)

Wanazuoni wengi — khususan Imam adh-Dhahabi katika Kitabu aAl-Kabair — wanaeleza madhambi makubwa kuwa ni yale ambayo:

Yameekewa adhabu maalumu duniani, au

Yametajwa kwa laana, ghadhabu ya Allah, au tishio la Moto.

☞ Haya ni miongoni mwa madhambi makubwa yaliyokubaliwa na wanazuoni wengi:

A. Kuhusu Itikadi na Ibada

1. Kumshirikisha Allah (Shirk)
2. Kukufuru / Kuacha Uislamu
3. Kuacha swala kwa makusudi
4. Kuacha kufunga Ramadhan bila udhuru
5. Kuacha kutoa Zaka bila udhuru
6. Kukataa nguzo za Uislamu
7. Kuapa kwa uongo kwa Jina la Allah

B. Kuhusu Nafsi na Maisha

8. Kuua bila haki
9. Kujitoa uhai (kujiua)
10. Kutoa ushahidi wa uongo
11. Kula mali ya yatima
12. Kula riba
13. Kula rushwa

C. Kuhusu Maadili na Jamii

14. Uzinzi (zina)
15. Ulevi na matumizi ya vitu vinavyolewesha
16. Ushoga / Liwati
17. Kufanya zinaa na ndugu wa karibu (incest)
18. Kufanya uchawi
19. Ufisadi wa ardhini (ufisadi ruhani na kimwili)

D. Kuhusu Haki za Watu

20. Wizi
21. Kula mali ya haramu kwa njia yoyote
22. Kudhulumu watu kwa maneno au vitendo
23. Kukata hukumu kwa dhuluma
24. Kuvunja ahadi kwa makusudi
25. Kuficha ushahidi wa haki

E. Kuhusu Familia

26. Kuwatukana wazazi
27. Kuwakatia wazazi uhusiano

28. Kutoridhia hukumu ya Allah katika ndoa
29. Kuwatolea wazazi lugha chafu (hata “ah”)
30. Kuwatupia wake zinaa bila ushahidi (Qadhf)

F. Kuhusu Uhusiano kwa Watu na Jamii

31. Fitna na uchochezi wa damu
32. Ghiba (kumsengenya mtu)
33. Namima (kuchochea maneno)
34. Kiburi (kuikataa haki na kudharau watu)
35. Kujiona na kujivuna
36. Kuidharau Qur’ani au Sunna
37. Kusema uongo juu ya Mtume ﷺ

G. Kuhusu Tabia Binafsi

38. Ukafiri wa neema
39. Kukataza mema na kuamrisha mabaya
40. Kutojali madhambi unayoyafanya (istiqrar)

MADHAMBI MADOGO (SAGHAIR)

Haya ni madhambi ambayo:

Hayana adhabu maalumu katika Qur’an au hadithi,

Hayajapata laana au tishio kali sana,

Hayajafikia kiwango cha kuharibu kabisa uhusiano wa mtu na Mola wake au dini yake.

Madhambi Madogo (kulingana na wanazuoni kama Ibn Qayyim na Imaam An-Nawawī):

A. Madhambi ya ulimi

1. Kufanya mzaha wa kupitiliza
2. Kusema maneno yasiyo na faida
3. Kusema nusu-uongo (si udanganyifu mkubwa)
4. Kukuza jambo kuliko lilivyo (exaggeration)

B. Madhambi ya macho

5. Kuangalia haramu bila nia mbaya mara ya kwanza (inapozidi huwa kubwa)
6. Kuangalia anasa au vitu visivyo na faida

C. Madhambi ya masikio

7. Kusikiliza mazungumzo yasiyo na faida
8. Kusikiliza mambo ya haramu kwa bahati mbaya bila makusudi

D. Madhambi ya moyo

9. Kufikiria mabaya juu ya watu (dhana) bila ushahidi
10. Hasira za haraka zisizofikia dhuluma

E. Madhambi ya viungo

11. Kutoswali sunna mara kwa mara
12. Kutoa sadaka ndogo kwa kiburi
13. Kuvunja Sunnah ndogo kama kula bila bismillah
14. Kuchelewa katika ibada bila sababu

F. Kuhusu jamii

15. Kutokutoa salamu
16. Kutokumjibu anayekusalimia

17. Kumdharau mtu kwa ishara ndogo
18. Kupitiliza mzaha hadharani

MUHIMU:

✓ Madhambi makubwa hutubiwa kwa toba maalumu:

Kujuta

Kuacha kabisa

Kuazimia kutorudia

Kurudisha haki za watu inapohitajika

✓ Madhambi madogo hufutwa na:

Swala tano

Ijumaa hadi Ijumaa

Ramadhan hadi Ramadhan

Dhikr (Utajo wa Allah)

Kufanya mema mengi

✓ *ZINGATIA TENA:*

🔹Madhambi makubwa ni yale yaliyotajwa katika Qur’ani au Sunnah kwa adhabu kali, laana, au tishio la Moto.

🔹Madhambi madogo husamehewa kwa ibada za kila siku, lakini yanaweza kuwa makubwa yakirudiwa sana au yakifanywa bila kujali.

Toba ndio kinga muhimu zaidi kwa muumini.

Tunamuomba Allah Subhaanahu Wataala Atukinge na Madhambi hayo Aamiin.

NJIA ZA KUYAFIKIA MAISHA MAZURI

Hakuna shaka kuwa kila mmoja wetu anatafuta, anapenda, na ana hamu kubwa ya kuishi maisha mazuri. Lakini vipi yanapatikana?

Watu wametofautiana kwa mitazamo na katika kuyatafuta maisha mazuri, kila mmoja ana mtazamo na njia zake yeye mwenyewe anaona anaweza kuyafikia:

Wako wanaotafuta maisha mazuri katika kukusanya mali na mtazamo wao ni kuwa maisha mazuri yatapatikana tu kwa wingi wa mali zao!

Wako wanaotafuta maisha mazuri katika michezo na kupoteza muda katika mambo yasio na faida!

Bali wako vile vile wanaotafuta maisha mazuri katika kumuasi Allah katika starehe za ulevi, zinaa n.k

Hakika Allah (Subhanahu Wataala) Muumba, Muendeshaji na Msimamiaji wa huu ulimwengu wote na vyote vilivyomo Ametaka na Amehukumu kuwa maisha mazuri ya kweli yatapatikana kwa kufuata njia na muongozo Wake na dhiki na usumbufu kwa yeyote atakae muasi na kupuuza utajo na muongozo wake!

Allah Subhanahu Wataala Amesema: ‘‘Na Atakaepuuza na kujieka mbali na utajo wangu basi kwa hakika

atakuwa na maisha ya dhiki (tabu) na tutamfufua siku ya kiyama akiwa kipofu’’ Qur’ani [20:124].
Hizi hapa ni baadhi ya sababu zinazopelekea maisha mazuri na furaha ya moyo katika maisha yote!
1- **IMANI SAHIHI NA MATENDO MEMA**
Imani Sahihi na Matendo Mema ndio sababu ya asili na msingi ya maisha mazuri na furaha ya kweli.
Allah (Subhanahu Wataala) Amesema:
"Mwenye kufanya matendo mema, mwanamme au mwanamke, akiwa ni muumini, basi tutamfanya aishi maisha mazuri na tutawalipa malipo yao kwa uzuri zaidi kutokana na yale mazuri waliokuwa wakiyafanya (duniani)" Qur’ani [16:97].
2- **KUMTEGEMEA ALLAH *PAMOJA NA KUFUATA SABABU, KWA KUJISHUGHULISHA NA KAZI MIONGONI MWA KAZI ZA HALALI AU ELIMU MIONGONI MWA ELIMU ZENYE MANUFAA.***
Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema katika hadithi sahihi kuwa:
"Lau munamtegemea Allah (Subhanahu Wataala) ukweli wa kumtegemea, basi Angewaruzuku kama Anavyowaruzuku ndege, ***wanatoka*** (asubuhi mapema) matumbo yao yakiwa matupu na wanarudi (jioni) wakiwa wameshiba" [Hadithi Sahihi].

3- **KUMTAJA SANA ALLAH**

Allah (Subhanahu wataala) Amesema:

"Na Allah Anawaongoza wale walioamini ambao nyoyo zao zimetulia kwa kumkumbuka (kumtaja) Allah, Tambua kuwa kwa utajo wa Allah kunazifanya nyoyo zitulie, Wale walioamini na wakafanya matendo mema watakuwa na furaha, kitulizo cha macho, hali nzuri na marejeo mema kwenye hizo Pepo za Allah na Radhi Zake" Qur'ani [13:28-29].

4- **Kuwafanyia wema viumbe wa Allah** kwa maneno (mfano: kuamrisha mema na kukataza maovu, kumtolea salamu unayemjua na usiemjua) na vitendo (kuwasaidia katika shida na haja zao), Kuunga udugu, koo, kupatanisha waliohasimiana, kuchanganyika na watu na kushirikiana nao katika furaha (harusi, mahafali n.k) na huzuni (misiba n.k), kuondosha sababu za hamu na huzuni na kufanya mambo yanayoleta furaha na uchangamfu, kuacha kufikiria mambo yaliyopita na kushughulika na mambo yaliyopo, kumtazama aliye chini na kuacha kuwafikiria walioneemeshwa zaidi katika mambo ya kidunia badala yake wafikirie wale uliowazidi kwa afya, uzima na neema nyengine hapo ndio utaiona neema ya Allah kwako, itapelekea kumshukuru.

Tunamuomba Allah Atuingize katika waja wake wenye kushukuru na atutoe katika waja wake wenye kukufuru Aamin.

TOBA YA KWELI

Toba (kutubia) maana yake ni kurejea kumtii Allah (Subhanahu Wataala) baada ya kuwa unamuasi.

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema:

"Rejeeni kwa Mola wenu nyote enyi mlioamini ili mupate kufaulu" Qurani [24:31].

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema;

"Sema, Ewe Muhammad kuwaambia waja wangu waliojidhulumu nafsi zao kwa kuyajia madhambi ambayo nafsi zao zinawaitia kwamba msikate tamaa na rehema ya Allah kwa wingi wa madhambi yenu, kwani Allah Anasamehe dhambi zote (kwa mwenye kutubia kutokana nayo na akayaacha namna yatakavyokuwa kabla hajaaga dunia). Hakika Allah ni mwingi wa kusamehe madhambi ya wenye kutubia miongoni mwa waja wake, ni mwenye kuwarehemu (bila kuangalia ukubwa na uzito wa dhambi)" Qur'ani [39:53].

Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema:

"Allah Anafurahi zaidi kwa kutubia mja wake kuliko furaha ya mmoja wenu aliyempata mnyama wake aliyepotea katika ardhi ya jangwa!" [Hadithi Sahihi].

Aya na Hadithi Sahihi zilizokuja kuonyesha upole, huruma na furaha ya Allah kwa waja wake wenye kutubia zipo nyingi na wala haziwezi kuingia hapa na katika hizo ni hadithi sahihi inayosimulia tukio la mtu aliyefanya ukatili wa kuuwa watu 100 kwa makusudi

lakini alipoamua kweli kweli kurudi kwa Allah, Allah Mwingi wa rehema Alimpokea na kumsamehe.

WANACHUONI WAMESEMA:
Toba ni lazima kwa kila dhambi anayofanya mja ikiwa ndogo au kubwa, ikiwa dhambi ni baina ya mja na Mola wake haiambatani na haki ya mja mwengine basi ina masharti matatu nayo ni:
1- Kuacha/kujiepusha na ile dhambi:
Mja anapotaka kutubia lazima kwanza aachane kabisa na ile dhambi, mfano kama ni mlevi au mzinifu aache ulevi au zinaa halafu ndio afikirie kutubia kama atatubia lakini bado anaendelea na ile dhambi toba yake haitakubaliwa.
2- Kujuta kutokana na dhambi aliyotenda, mfano kama amezini na anataka kutubia kwanza aache halafu ajute kwa nini ameingia katika dhambi hiyo na ikiwa yatamtoka machozi, hiyo ndiyo ishara kubwa ya kukubaliwa toba yake kwa sababu machozi yanafuta madhambi kama maji yanavyozima moto.
3- Kuazimia kutorejea tena katika dhambi aliyotenda, mfano kama amezini kwanza aachane na zinaa pili ajute kwa nini amezini na mwisho aazimie kwamba hatorejea tena katika maisha yake yote. Zikitimia sharti hizo kwa dhambi iliyo baina yake na Mola wake basi toba yake itakubaliwa ikikosekana sharti moja tu toba yake haitakubaliwa.

Ikiwa dhambi aliyotenda ni baina yake, Mola wake na mtu mwengine basi inaongezeka sharti ya nne nayo ni kujitakasa kutokana na haki yake:

Ikiwa amemdhulumu kwa kuchukua mali yake basi amrejeshee.

Ikiwa amempiga au kumtukana basi amuombe msamaha.

Ikiwa amemsengenya au amemsingizia basi amuombe amhalalishie au amsamehe n.k.

Toba ni mlango mkubwa wa rehema ya Allah Subhanahu Wataala unaofunguliwa kwa kila aliyekosea bila kujali ukubwa wa kosa lake.

Umuhimu wake upo katika kusafisha moyo wake, kurejesha matumaini na kumrudisha mja katika nuru ya uongofu baada ya giza la upotofu.

Kupitia toba mja hujifunza unyenyekevu, hutambua udhaifu wake na huimarisha uhusiano wake na Mola wake jambo linaloleta amani na furaha ya moyo na mabadiliko ya kweli ya tabia.

Hakika toba ya kweli ni mwanzo mpya wa maisha yenye baraka na radhi za Allah Subhanahu Wataala

Tunamuomba Allah (Subhanahu Wataala) atukubalie toba zetu na atusamehe dhambi zetu na Atupe mwisho mwema Aamiin.

HAKI YA ALLAH (SUBHANAHU WATAALA)

Allah (Subhanahu Wataala) Ametuumba kwa lengo kuu maalum nalo ni:
KUMUABUDU BILA KUMSHIRIKISHA NA KITU CHOCHOTE.
Allah (Subhanahu Wataala) Amesema:
"Sikuwaumba Majini na Watu isipokuwa waniabudu, Sitaki riziki kutoka kwao wala sitaki wanilishe, kwa hakika Allah Ndiye Mtoaji wa riziki, Mwenye nguvu madhubuti" Qur'ani [51:56-58].
Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema:
"Haki ya Allah kwa waja wake ni kumuabudu bila kumshirikisha na chochote na Haki ya waja kwa Allah ni kwamba asiwaadhibu iwapo watamuabudu bila kumshirikisha na chochote" [Hadithi Sahihi].

MAANA YA IBADA

IBADA ni kila anachokipenda na kukiridhia Allah katika maneno na vitendo vya wazi na siri (moyoni). Kila anachofanya MJA عبد kinaweza kuwa IBADA العبادة yenye ujira iwapo atakifanya kwa ajili ya Bwana wake Ambae ni Allah na kwa utaratibu anaotaka Yeye nao ni utaratibu wa Mtume wetu Muhammad (Swallallahu Alaihi Wasallam).
Allah (Subhanahu Wataala) Amesema: "Sema Ewe Mtume: Hakika Swala yangu na Ibada zangu (nyengine zote ikiwemo kuchinja) na Uhai wangu (kula, kulala,

kuamka, kufanya kazi n.k) na kufa kwangu ni kwa ajili ya Allah Bwana wa viumbe vyote"
"Asiye na mshirika (katika Uumbaji, Uendeshaji, Usimamiaji, Uungu-kuabudiwa, Utukufu, Ufalme, Sifa na Dhati zake) na hivyo kumpwekesha Allah katika Mambo yake yote ndivyo nilivyoamrishwa (na Mola wangu) na Mimi ni wa kwanza katika wale wenye kujisalimisha kwa kufuata yale yote Anayotaka Allah katika umma huu wa mwisho"
"Sema Ewe Mtume: Je, nishike Mola mwengine asiyekuwa Allah, na hali Yeye (Allah) ndie Mola (Muumba, Muendeshaji na Msimamizi) wa kila kitu..." Qur'ani [6:162-164].
Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) Amesema: "Hakika (Si vyenginevyo) matendo hufanywa kwa nia (yaani haiwezekani kufanya kitendo bila nia-kukusudia) na kwa hakika kila mtu atalipwa kwa kile alichokinuia-alichokusudia.." [Hadithi Sahihi].
Hadithi inafahamisha kuwa Allah (Subhanahu Wataala) Analipa Matendo yaliyofanywa kwa ajili yake na Hahusiki kabisa na kulipa matendo yaliyofanywa kwa ajili ya mwengineo yeyote asiekuwa Yeye!
Hivyo Ndugu yangu katika imani kama unaswali (Swala tano), unasoma elimu yoyote yenye manufaa, Unafanya kazi ya halali, Unasaidia watu wako na jamaa wa karibu, Unasaidia Jamii iliyokuzunguka kwa namna yoyote kielimu, kifedha, ushirikiano na nguvu kazi n.k tuhakikishe tunahudhurisha "NIA" katika"MOYO" Kwamba tunafanya yote haya kwa ajili ya kutafuta Radhi za Allah pekee! na hapo tu ndio Allah Atatulipa

ujira wetu kamili siku nzito ya kiama na wala tusithubutu kabisa kufanya matendo mema kwa ajili ya watu au mali au cheo, halafu tukatarajia kupata malipo kutoka kwa Allah Muumba, Muendeshaji, Msimamiaji na Mfalme wa mbingu saba na ardhi saba na vyote vilivyomo baina yake! ili tusije tukawa katika wale watakaomuendea Allah Siku nzito ya kiyama kudai malipo yao wakiwa na matendo mengi ya kheri mfano wa majabali!
Allah Atawajibu kwa uadilifu kuwa "Mimi nalipa malipo ya matendo yaliyofanywa kwa ajili Yangu! nyinyi waja wangu hamukufanya kwa ajili yangu kwa hivyo nendeni kwa hao muliofanya matendo yenu kwa ajili yao ili wakulipeni ujira wenu muone kama mutapata ujira wowote!" (Mafhum ya Hadithi Sahihi)
Uislamu ni Mfumo kamili wa maisha kwa maana kila kitu anachofanya mja ndani ya masaa ishirini na nne tayari kimebainishwa na kuekewa utaratibu wake vizuri katika Qur'ani na Hadithi Sahihi za Mtume kwa maslahi ya Mwanadamu ya kiroho na kimwili.
Tunaomba Allah (Subhanahu Wataala) Atuongoze katika njia sahihi iliyonyooka, Aamin.

HAKI ZA MTUME (SWALLALLAHU ALAIHI WASALLAM) KWA UMMA (WAFUASI) WAKE

KUMUAMINI
Muislamu anatakiwa amuamini Mtume kwa kila anachokisema kwa sababu Yeye hatamki kwa matamanio isipokuwa ni Wahyi kutoka kwa Mola wake.

KUMTII
Allah (Subhanahu Wataala) Amesema: "Kama mtamtii basi mutaongoka"
"Atakaemtii Mtume basi kwa hakika amemtii Allah".
KUMPENDA
Mtume Amesema " Hatoamini mmoja wenu mpaka mimi niwe napendeza zaidi kwake kuliko wazazi wake, watoto wake na watu wote" (Hadithi Sahihi).
KUMUIGIZA
Allah (Subhanahu Wataala) Amesema:
"Hakika mumekuwa na kigezo chema kwa Mjumbe wa Allah (Subhanahu Wataala)..."
KUMSWALIA
Mtume Swallallahu Alaihi Wasallam Amesema:
"Mwenye kuniswalia mara moja Allah Subhanahu Wataala humswalia mtu huyo mara kumi (10)".
KUMUOMBEA DUA
Amesema Mtume "Mtu yeyote atakaye muombea dua baada adhana ataupata uombezi wake"
KUHUISHA SUNNA ZAKE
Sunna zake ni kila kauli au kitendo kilichopokelewa kutoka kwake.
KUWAPENDA MASWAHABA WAKE
Katika kuwapenda ni kutozungumzia sana kuhusu tofauti zilizotokea baina yao, kuwaombea dua na kutokubali mtu yeyote kuwashusha hadhi zao kwa kuwadhalilisha na kuwatukana.
KUIFAHAMU SIRA YAKE
Inamsaidia muislamu kuishi katika manhaj (njia) yake katika nyanja zote za maisha mfano Akiwa mtoto,

akilingania, mwanafunzi, mwalimu, mfanya biashara, mume, baba akiwa kama kiongozi wa dola, akiwa amiri jeshi n.k.

KUTHIBITISHA KAULI ZAKE

Apambanue kauli zilizo sahihi na zile dhaifu na za kuzusha.

KUMNUSURU

Kwa kuunusuru uislamu, kumfuata, na kuhuisha sunna zake.

KUWAKIRIMU WATU WA NYUMBANI KWAKE

Aliwahi kuwakumbusha wafuasi wake juu ya kuwakirimu-kuwaheshimu bila kuchupa mipaka watu wake wa karibu mfano: Bibi Fatma, Sayyidna Ali, Sayyidna Hassan na Hussein.

HAKI ZA MUISLAMU

Ndugu/Dada yangu Allah Akurehemu, Mtume (Swallallahu Alaihi Wasallam) amezitaja haki sita (6) za Muislamu juu ya muislamu mwenzake kama ifuatavyo:

KUMTOLEA SALAMU ANAPOKUTANA NAYE

Salamu ni moja katika njia za kuongeza mapenzi na udugu baina ya waislamu. Mtume Amesema: "Hamtoingia peponi mpaka muamini (muwe na imani) na hamtoamini mpaka mupendane, Jee nikufahamisheni jambo ambalo mukilifanya mutapendana? Toleaneni salamu baina yenu" [Hadithi Sahihi].

KUMUITIKIA ANAPOMUALIKA

Kumuitikia muislamu katika mualiko ni haki ya muislamu kama alivyosema Mtume (Swallallahu Alaihi

Wasallam):
"Chakula kibaya zaidi ni chakula cha karamu wanaitwa wale wasiokihitaji (matajiri) na wanaachwa wale wanaokihitaji (masikini) na mwenye kuitwa basi aitikie wito" [Hadithi Sahihi].

KUNASIHIKA ANAPOMNASIHI:
Kumsikiliza na kukubali nasaha anapokunasihi ndugu yako muislamu ni katika haki zake za msingi kama ilivyokuja katika hadithi sahihi kwamba Mtume Amesema "Dini ni nasaha (kunasihiana)".

AMUOMBEE DUA ANAPOKWENDA CHAFYA
Kumuitikia muislamu mwenzako aliyekwenda chafya na akasema Alhamdulillah kwa kumwambia Allah Akurehemu ni katika haki za msingi za muislamu juu ya muislamu mwenzake.

KUMTEMBELEA ANAPOUMWA
Amesema Baraai ibn Aazib (Allah Amridhie): "Ametuamrisha Mjumbe wa Allah kumtembelea mgonjwa, kumfuata maiti (jeneza), kumuitikia mwenda chafya, kumnusuru mwenye kudhulumiwa, kuitikia wito na kutoa salamu" [Hadithi Sahihi].

KUMFUATA ANAPOKUFA:
Mtume Swallallahu Alaihi Wasallam Amesema: "Atakae hudhuria swala ya maiti mpaka iswaliwe, atapata Qirati moja, na atakaehudhuria mpaka maiti atakapozikwa atapata Qirati mbili" Akaulizwa: "Qirati mbili ni nini?"Akajibu "Ni thawabu zenye mfano wa majabali mawili makubwa" [Hadithi Sahihi].

Hizo ni haki za msingi za Muislamu juu muislamu mwenzake ni muhimu sana kuzichunga na kuzihifadhi ili tuishi vizuri na watu kwa kujaliana, kusaidiana, kuheshimiana, kustiriana, kusameheana na kupendana.

HAKI ZA WAZAZI

Allah Subhanahu Wataala Amesema:

“Na Amehukumu Mola wako kwamba musimuabudu yeyote isipokuwa Yeye tu na kwamba Wazazi wawili kuwafanyia wema, Pale watakapofikia wakiwa kwako uzee mmoja wao au wote wawili basi usiwaambie hata neno dogo la kuwadharau au kuwadogosha na wala usiwakaripie (kwa maneno makali) na useme nao maneno yaliyo mazuri (laini)” Qur’ani (17:23)

Miongoni mwa haki za wazazi ni kuwafanyia wema, kuwatii katika mambo ambayo si ya kumuasi Allah, kusikiliza maagizo yao, kuwaheshimu, kutowatangulia katika maneno au kutembea, kuwakidhia haja zao, kuwahurumia, kuwajali, kuwasamehe wanapokukera na kawaombea dua Allah Awasamehe na Awarehemu.

HAKI ZA MKE NA MUME KATIKA NDOA

Maisha ya ndoa yana adabu zake na haki zinazotakiwa kutekelezwa kwa pande zote mbili (mume na mke) nazo ni kuwa kila mmoja katika wana ndoa asimame katika kutekeleza haki za mwenzake ili yapatikane maelewano, maridhiano, utulivu, mapenzi na maisha yawe mazuri katika ndoa.

HAKI ZA MKE KWA MUME

Mume ni jukumu lake kumtafutia mke wake mahitaji ya lazima (basic needs): Chakula, Mavazi, Makazi kwa wema na moyo mkunjufu, aishi vizuri na mke wake, awe mpole, mlaini, mwenye bashasha, amfanyie upole anapokasirika na amridhie, amstahamilie na kumsamehe anapokosea na astahamili maudhi anayomfanyia na ampatie matibabu anapoumwa, amsaidie kazi nyumbani, amuamrishe kutekeleza faradhi zilizo juu yake kama vile swala, swaumu n.k na amkataze kufanya yaliyoharamishwa kwake.

Mume ni wajibu kumfundisha mkewe mambo yanayomlazimu katika dini yake na ibada zake, asimlazimishe mambo yaliyo nje ya uwezo wake, asimnyime au kumzuia kutafuta elimu yenye manufaa ikiwa yeye hawezi kumfundisha ikiwa hakuna uwezekano wa kutokea fitna.

Mume awaheshimu jamaa wa mkewe na asimzuie kuwa karibu nao.

Mume ni wajibu kumtekelezea mke wake haki ya tendo la ndoa kwa njia za halali kwa wakati wowote na katika hali yoyote ikiwa halitomdhuru tendo hilo au kumshughulisha asitekeleze jambo la faradhi na wala asimnyime anavyovipenda katika vitu vya halali.

Mume ni wajibu kumfanyia mke wake kile anachopenda kufanyiwa yeye na ikitokezea kufikia

hatua ya kumpiga basi ajiepushe kumpiga usoni, asimtukane, asimuhame isipokuwa katika kitanda tu, asimlaumu mbele ya watoto wake na wala asitoe aibu zake mbele ya watu wengine na kadhalika.

HAKI ZA MUME KWA MKE

Ni wajibu kwa mke kumtumikia mume wake, kuiweka vizuri nyumba kwa kuendesha mambo ya nyumbani, kuwalea vizuri watoto wao na kumnasihi kwa njia nzuri.

Mke anatakiwa ahifadhi heshima ya mume wake kwa kujihifadhi yeye mwenyewe, kuhifadhi mali ya mume wake na nyumba yake, ampokee kwa furaha, bashasha na uchangamfu na ajipambe kwa ajili yake.

Mke anatakiwa amheshimu mume wake na aishi naye kwa wema na amuitikie anapomuhitaji kwa ajili ya tendo la ndoa, na afanye kila linalotia furaha katika moyo wake ili upatikane utulivu, mapenzi, furaha na mafanikio katika maisha yao ya ndoa.

Mke ni wajibu kumtii mume wake katika mambo ambayo si ya kumuasi Allah ikiwa atamuarisha katika maasi basi asimtii kwa sababu "Hakuna kumtii kiumbe katika kumuasi Muumba".

Mke anatakiwa asitoke katika nyumba bila rukhsa ya mume wake, ajiepushe na mambo yanayomuudhi mfano: Asionyeshe furaha wakati wa huzuni na huzuni wakati wa furaha, asimuudhi kwa kutumia ulimi wake,

asitoe siri zake kwa mtu yeyote, asitumie mali yake kwa fujo bila rukhsa yake, asimuingize katika nyumba mtu asiyempenda, awaheshimu jamaa zake na amsaidie kwa kiasi cha uwezo wake wakati anapoumwa au kupatwa na mitihani n.k.

Kwa hivyo hapa tunapata kujuwa kuwa mwanamke akiwa nyumbani anatekeleza majukumu makubwa kwa ajili ya mume wake na jamii kwa ujumla ambayo hayaingiliani na majukumu anayotekeleza mume wake nje ya nyumba kama kwamba mwanamke ni waziri wa mambo ya ndani na mwanamme ni waziri wa mambo ya nje. Hivyo wale wanaotaka kumtoa katika nyumba yake ambayo ndio sehemu ya majukumu yake ili ashirikiane kwa kusongamana na wanaume katika majukumu yao ya nje wamepotea upotevu wa wazi na wamepoteza wengi katika kuharibu familia na jamii zao.
Allah (Subhanahu Wataala) Amesema kuwaambia Waumini wanawake:
"Na jilazimisheni kukaa majumbani mwenu (msitoke humo isipokuwa kwa mahitaji) na msionyeshe uzuri wenu kama vile wanawake wa kipindi cha ujinga wa mwanzo walivyokuwa wakifanya.." Qur’ani [33:33].

Mke anatakiwa afuate muongozo ufuatao katika kumpokea mume wake: Mume anapotoka kazini,

safarini au popote pale palipowatenganisha, aanze kwa maamkizi mazuri, ampokee kwa uso mchangamfu, ajipambe na ajitie manukato, aanze kwa habari nzuri na acheleweshe habari yoyote mbaya mpaka atakapokwisha pumzika, ampokee kwa maneno matamu ya mapenzi na shauku, afanye vizuri katika mapishi na akitayarishe kwa wakati, aipambe na ailainishe sauti yake kwa ajili ya mume wake, ukifika wakati wa jimai mwanamke ahakikishe yuko safi katika hali zote, ahudhurishe fikra na hisia zake katika tendo hilo, asijifanye hana hamu, kuona haya na kujifanya haathiriki. Akishikwa panapomfanya ashituke basi ashituke, akishikwa panapomfanya alegee basi ajilegeze, akishikwa panapomfanya atekekenyeke basi atekenyeke na akishikwa panapomfanya alewe basi alewe na awe mbunifu wa kutafuta njia za kumtuliza na kumfurahisha mume wake.

Ni haramu kwa yeyote kati ya mume au mke kwenda kinyume kwa kuacha kumtekelezea mwenzake haki zake zilizo juu yake na matokeo ya kufanya hivyo ni mipasuko katika familia ambayo itapelekea chuki, uhasama na fitna katika jamii nzima kwa sababu familia ndio zinazounda jamii na jamii ndio zinazounda nchi.

Tunamuomba Allah Subhanahu Wataala Atie nuru ya Uislamu katika majumba na familia zetu, Aamin.

UJUMBE WA MWISHO

Ujumbe wa Mwisho wa kitabu hiki ni kuwa ili kutengeneza, kunufaika, kuimarisha na kuhifadhi Imani zetu katika zama hizi tunalazimika tufungamane na tushikamane na Qur'ani tukufu kwa wingi wa kuisoma, kuisikiliza, kuifundisha, kuizingatia na kuifanyia kazi pamoja na Hadithi Sahihi za Mtume Swallallahu Alaihi Wasallam.

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema:

"(Hakika hii Qur'ani ni) Kitabu Tumekiteremsha kwako [Ewe Mtume] chenye baraka nyingi ili watu wazingatie aya zake na wakumbuke wenye akili" Qur'ani [38:29].

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema:

"Lau kama tungeiteremsha hii Qur'ani katika jabali, hakika ungeliona linanyenyekea na kupasuka kutokana na khofu ya kumuogopa Allah. Hiyo ni mifano tunaipiga kwa ajili ya watu ili wapate kutafakari" Qur'ani [59:21].

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema:

"Hakika hii Qur'ani inaongoza katika yale yaliyo sawa na kweli na inawapa habari njema waumini ambao wanafanya matendo mema kwamba watakuwa na ujira mkubwa" Qur'ani [17:9].

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema:

Na tumeteremsha katika Qur’ani yale ambayo ni ponyo (tiba) na rehma kwa waumini wala haiwazidishii (hii Qur’ani wanapoisikiliza waliodhulumu) isipokuwa hasara” Qur’ani [17:82].

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema:

"Enyi watu yamewajia mawaidha (Qur'ani) kutoka kwa Mola wenu na tiba (dawa) ya yale yaliyomo vifuani (nyoyoni katika maradhi), na mwongozo na rehema kwa waumini (wenye imani)" Qur’ani [10 :57].

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema:

“Kila nafsi itaonja mauti na kwa hakika mutalipwa malipo yenu kamili siku ya kiyama, basi yule atakayeepushwa na moto na akaingizwa katika pepo kwa hakika amefaulu na hayakuwa maisha ya dunia isipokuwa ni starehe fupi yenye kudanganya” [3:185].

Aya hiyo iliyotangulia [3:185] ni nzito sana na imegusia mambo mengi lakini tueleze kwa ufupi kuhusu uchungu wa mauti ambao kila mja lazima atauonja na muda wote uko karibu mno na mwanadamu yeyote!

Uchungu wa mauti ni maumivu makali sana, shida na hali ngumu sana anazopitia mja anapokaribia kufariki dunia. Hiki ni kipindi cha mwisho cha uhai wa mtu duniani kabla ya roho yake kutolewa na malaika wa

mauti. Katika uchungu wa mauti kuna mambo mengi sana katika hayo ni hili lifuatalo kwa ufupi:

Hali ya maumivu makali

Mauti si jambo jepesi, ni wakati ambao roho inatolewa mwilini. Hali hii huchukuliwa kuwa yenye uchungu sana kama vile kuchanwa au kung'olewa kitu kilichoingia kwenye mwili mzima.

Maulamaa wameeleza uzito wa hali hiyo kwa kusema:

"Mauti (kifo) yana maumivu makali zaidi kuliko maumivu ya mapanga elfu moja kupigwa mara moja"

Maneno hayo yana maana kuwa hakuna maumivu yoyote katika dunia hii yanayoweza kukaribiana na maumivu ya mauti.

Amesema Imaam Nasir Ibn Muhammad Samraqandy:

Mwenye kuwa na yakini juu ya mauti na akawa anajua kuwa lazima yatamfika, basi lazima atajiandaa kwa kufanya matendo mema na atajiepusha na matendo maovu kwa sababu hajui ni wakati gani na hali gani na pahala gani yatamfika!

Mtume Swallallahu Alaihi Wasallam Amebainisha kuwa:

"Fanyeni wingi wa kukumbuka kitu kinachovunja

utamu wa uhai (mauti)” ili muda wote tujiandae na tuwe na subra katika kukabiliana na shida za kidunia kwa sababu shida na mashaka ya kidunia ni mepesi sana kuliko shida ya mauti kwa sababu mauti ni katika adhabu za akhera na adhabu za akhera ni kubwa kuliko adhabu za duniani.

Kwa hivyo ni lazima kila muislamu ajiandae na mauti wakati wote kwa kufanya matendo mema akiwa muumini wa kweli na kujiepusha na maasi yote makubwa na madogo, hii ndio salama kwa yeyote yule ambae anatarajia kukutana na Mola wake. Ni bora mara elfu kustahamili tabu ya muda mfupi ya duniani kuliko tabu ya maisha ya milele yasiyo na mwisho!

Tunamuomba Allah Subhanahu Wataala Atupe mwisho mwema, Aamiin.

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema:

“Enyi Mlioamini (Wenye Imani ya kweli) Mcheni Allah (Subhanahu Wataala) na iangalie nafsi nini imetanguliza (katika matendo) kwa ajili ya kesho, na Mcheni Allah (Subhanahu Wataala), Hakika Allah ni Mjuzi wa yote munayoyafanya” Qur’ani [59:18].

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema:

“Na iogopeni siku ambayo mutarejeshwa katika siku hiyo kwa Allah (Subhanahu Wataala) kisha ilipwe kila nafsi ilichochuma na wao hawatodhulumiwa” [2:281].

Allah (Subhanahu Wataala) Amesema:

“Naapa [(Allah Subhanahu Wataala) Anaapa] kwa zama (wakati), Hakaika mwanadamu (yeyote) yumo katika khasara (ya kuangamia), isipokuwa (hawamo katika khasara) wale walioamini na wakafanya matendo mema na wakausiana kushikamana na haki (kheri zote) na wakausiana kushikamana na kusubiri (katika kutekeleza maarisho, kuacha makatazo, maradhi, misiba, mabalaa, maudhi ya watu na kadhalika)” Qur’ani, Surat Al-Asr [103 :1-3].

DUA

Tunamuomba Allah Subhanahu Wataala Akijaalie kijitabu hiki kiwe swadaka yenye kuendelea kwa yeyote atakayefaidika kwa kusoma, kuzingatia, kufanyia kazi na kusambaza kwa njia yoyote.

Tunamuomba Allah Subhanahu Wataala Akijaalie kijitabu hiki kiwe kimekusanywa na kuandikwa kwa kutafuta radhi zake tu si kwa lengo jengine lolote lile na Atusamehe pale tulipokosea katika kufikisha. Ewe Mola Wetu tukubalie matendo yetu hakika yako Wewe

ni Mwenye Kusikia (maombi yetu) na Mwenye Kujua (nia zetu).

Ewe Mola Wetu tuondoshee unafiki, shaka, kiburi, husda, kujiona na kujionyesha katika nyoyo zetu.

Ewe Mola Wetu zipambe nyoyo zetu kwa Imani na Uchamungu na tujaalie tuwe katika waja wako wema walioongoka.

Ewe Mola Wetu Wasamehe na Warehemu Waumini na Waislamu Wanaume na Wanawake walio hai na waliotangulia kwako, Aamin Yaa Rabbal Aalamiin.

MAREJEO YA VITABU

Qur'ani Tukufu na Tafsiri yake

Imani, Nguzo zake, Uhakika wake na Vitenguzi vyake, [Sheikh Muhammad Naem Yasin]

Misingi ya Imani, Kundi la Wanachuoni

Kitabu cha Imani, Ibn Taymiya

Kitabu cha Imani, Swahihi Bukhari, Imam Bukhari

Kitabu cha Imani, Swahihi Muslim, Imam Muslim

Nuru ya Imani, Ibn Wahf Al-Qahtwany

Visa vya Mitume, Mwanzo na Mwisho, Ibn Kathir

General Astronomy, en.wikibooks.org (2015)



Kimekamilika Kitabu cha Nuru ya Imani (Furaha ya Moyo) kwa rehema na uwezo wake Allaah Subhaanahuu Wataala. Mwisho wa Maombi Yetu Waislamu ni Kusema

Alhamdulillaahi Rabbil Aalamiin